**LHRC** yaanika siri wanawake uongozi vyombo vya habari

UKURASA 18



**Majaliwa** apongeza Watanzania kwa kushiriki kongamano la Urusi

UKURASA 19




UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatatu Julai 31, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581388

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# CCM, CHADEMA sasa jino kwa jino

• **Wanyukana** mikoani sakata la Bandari, Lissu atoa utabiri Uchaguzi Mkuu 2025; Mbowe, Chongolo hapatoshi... *Endelea ukurasa 2*



Ibara ya 5(iv) ya mkataba imeeleza ikitimia miezi 12 tangu kutiwa saini mkataba huo Oktoba 22, 2022, kama hawajafika mwafaka wa miradi, basi mkataba huo utakuwa umefika ukomo.

**SILAA**



Ili tuendelee kuitetea haki katika nchi yetu, tunahitaji uungwaji mkono wa wananchi kwa kuwa chama hiki ni chenu, kilindeni kwa nguvu zote.

**MBOWE**



Mkataba huu sio msahafu wala Biblia kusema kuwa hauna dosari kwani umeandikwa na wanadamu.

**CHONGOLO**



Wanasema mkataba utaisha pindi tu wawekezaji watakapomaliza shughuli zao za uboreshaji, hapa tukumbuke shughuli hizi haziishi hadi ziwa na bahari vikauke.

**LISSU**

MIFUGO HIFADHINI

## Korti Kuu yaamuru waliopigwa faini warejeshewe fedha

UKURASA 3

## Kicheko kwa wakulima serikali ikinunua mahindi kwa bei nzuri

UKURASA 19

**MICHEZO** **SIMBA KUMTEMA KIPA MBRAZILI** UK.24

**KATUNI** UK.6

# CCM, CHADEMA jino kwa jino mikoani

**Vitus Audax na Elizabeth Zaya**

CCM na CHADEMA sasa jino kwa jino. Wakati Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kikiendelea na mikutano yake Kanda ya Ziwa kupinga mkataba wa uboreshaji ya Bandari baina ya Tanzania na Kampuni ya DP World ya Dubai, Chama Cha Mapinduzi (CCM) nacho kimeongeza nguvu katika kanda hiyo kuhakikisha kinaelimisha wanachama na wananchi kuhusu umuhimu wa mkataba huo.

Licha ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana kuwa na mikutano hivi karibuni katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, jana Katibu Mkuu wa chama hicho, Daniel Chongolo, alifanya mkutano mkubwa mkoani Mwanza, hoja kubwa ikiwa utekelezaji wa mkataba huo.

Chongolo pia anatarajiwa kuwa na kikao kazi leo na madiwani wote wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, moja ya ajenda ikiwa ni suala hilo hilo la bandari ili kuwawezesha kutoa elimu hiyo kwa wananchi katika ngazi zao za kata.

Katika hotuba yake jana mkoani Mwanza, Katibu Mkuu Chongolo aliitaka serikali kufanya marekebisho katika maeneo yenye tija katika mkataba huo wa uwekezaji na kuhakikisha yanafanyiwa kazi haraka ili utekelezaji uanze mapema.

"Sisi Chama Cha Mapinduzi tunaiagiza serikali kuhakikisha inatekeleza suala hili la marekebisho kwa kufanya mapitio na kuangalia mazingira na kuona umuhimu wa kuuhusu mawazo yenye tija ili kutufikisha ambapo tutapata tija.

"Tunasema hivi kwa sababu mkataba huu sio msahafu wala Biblia kusema kuwa hauna dosari kwani umeandikwa na wanadamu na macho yanatofautiana na elimu vilevile, inafanya watu waweze kuona mambo tofauti, hivyo maoni yachukuliwe," aliagiza.

Kuhusu kero za wananchi, Chongolo alizitaka mamlaka kuhakikisha zinaongeza kasi katika utatuaji wa kero hizo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha huduma za kijamii; maji, elimu, afya, umeme na miundombinu zinapatikana.

Katika mkutano huo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema lengo la kumkaribisha mwekezaji huyo nchini ni kuondoa ukiritimba katika bandari na kuboresha utendaji kazi bandarini.

Alisema kupitia uwekezaji huo mapato yataongezeka kutoka Sh. trilioni 7.7 yanayokusanywa na TRA hadi kufikia Sh. tirioni 26 ifikapo mwaka 2032/33 huku Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Jerry Silaa akisema Bunge liliridhia mkataba huo kwa mujibu wa katiba ya nchi ibara ya 63.

Kuhusu ukomo wa mkataba, Silaa alisema Ibara ya 5(iv) ya mkataba huo imeeleza kuwa ikitimia miezi 12 tangu kutiwa saini mkataba huo Oktoba 22, 2022 kama hawajafikia mwafaka wa miradi, basi mkataba huo utakuwa umefika ukomo.

Mwasisi wa Kampuni ya TICS ambayo ilikuwa na zabuni ya kuendesha shughuli za bandari, Nazir Karamagi, alikanusha kampuni hiyo kutokufanya vyema, huku akiunga mkono mkataba mpya baina ya serikali na kampuni ya Dubai.

**CHADEMA**

Wakati hali ikiwa hivyo CCM, CHADEMA jana waliendelea na mikutano yao ya 'Operesheni +255 Katiba Mpya Okoa Bandari Zetu' katika Wilaya za Muleba, Missenyi na Karagwe na Kyerwa, mkoani Kagera. Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Freeman Mbowe, akiwa Kata ya Mabira, wilayani Kyerwa aliwaomba wananchi kuendelea kukiamini chama hicho katika kutetea maslahi ya nchi.

"Ili tuendelee kuitetea haki katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuiwajibisha serikali pale inapoenda kinyume hususani katika mkataba huu, tunahitaji uungwaji mkono wa wananchi kwani chama hiki ni chenu, hivyo kilindeni kwa nguvu zote," alisema Mbowe.

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Bara, Tundu Lissu, akiwa wilayani Muleba, aliwahimiza wananchi kuendelea kupinga mkataba huo kwa umoja, akisema kuwa tangu enzi za ukoloni bandari hizo zilipojengwa, uboreshaji umekuwa unafanyika hadi leo, hivyo mkataba huo unapaswa kuwa na ukomo.

"Wanasema mkataba utaisha pindi tu wawekezaji watakapomaliza shughuli zao za uboreshaji, hapa tukumbuke shughuli hizi haziishi hadi ziwa na bahari vikauke maana vikiwapo uboreshaji lazima ufanyike kila mara, hivyo hatuwezi kuukubali mkataba huu," Lissu alisema.

Pia alizungumzia kile alichokita utitiri wa ushuru kwa wazalishaji na wafanyabiashara ya kahawa na mfumuko wa bei ya sukari mkoani Kagera, akilitaja ni tatizo linatokana na mwingiliano wa mamlaka na wakulima hao.

UTABIRI 2025

Katika hatua nyingine, Lissu alisema kuwa mwaka 2025 utakuwa mwisho kwa CCM kuwa madarakani.

Mwanasiasa huyo mwenye taaluma ya sheria, alisema kuwa miaka 64 ya CCM kuwa madarakani inatosha (kutoka 1961-2025) na sasa ni wakati wa chama hicho kung`oka ifikapo 2025.

"Shida zote zinazojitokeza sasa zinasababishwa na CCM, na ndio maana tunasema mwaka 2025 ndio mwisho wake, inatosha!" Lissu alidai.

Alisema katiba mpya ndio itakuwa suluhisho la matatizo yote ambayo yamekuwa yanajitokeza nchini.

"Tutengeneze katiba mpya ambayo itazuia shida zote hizi ikiwamo ufisadi. 2025 iwe mwisho wa CCM kuongoza nchi hii, miaka 64 inatosha. Katiba mpya ndio suluhisho ili tuifanye Ikulu kuwa mahali patakatifu," alisema.

Lissu alisema "ili kumalizana na CCM, ni lazima kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji, kata, wilaya, mikoa hadi taifa".

Alifafanua: "Ikitushinda kumalizana na CCM kwenye miaka miwili ijayo, watatumaliza. Kwahiyo, ni ama zao ama zetu. Na tusipomalizana nao kwenye hii miaka miwili mambo yatakuwa mabaya zaidi," alidai Lissu.

Viongozi wa CHADEMA, wakiongozwa na Mbowe, wako mkoani Kagera, wakiendesha mikutano ya hadhara katika katika vijiji, kata na wilaya zote.



Mkurugenzi Msaidizi wa Usafiri wa Anga na Hali ya Hewa kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Biseko Chiganga, akitia saini mikataba ya makubaliano ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na Urusi katika hafla iliyofanyika nchini humo. Anayeshuhudia kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Sheria Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Maria Makalla Memba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


## TANGAZO LA MNADA

**REVACCO Services Limited** na Tulvin Investment Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari jijini Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Ramson Florian Kunambi | TOYOTA ALPHARD-T917DFR | 15.08.2023 |
| Moses Reward Nyange | TOYOTA COASTER- T973 DLX | 15.08.2023 |
| Said Khalid Kisokola | TOYOTA COASTER -CHW 1777 | 15.08.2023 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano piga**
**0686908882 (Tulvin) au**
**0677014355 (Fanikiwa)**
**0717935186(Revacco)**

117528501



## KUPOTEA KWA VYETI



**Kondwani John Mchosa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **S1450-0045** cha Efatha Seminary School mwaka 2015. Cheti cha Technician Certificate in Records Archives and Information Management NTA Level 5 chenye Registratin **No. DRM.09/19/DSM.558** cha Tanzania Public Service College mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/253242/2023.**



## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NICKSONI SANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI ILIYOSAJILIWA JINA FELIX CHESCO MHAMILAWA,USAJILI NAMBA **MC530 CMQ,** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE JALADA NAMBA **MOR/MOR/RB/412569/2022.**



## KUPOTEA KWA KADI YA GUTA

**AUGUSTINO OBADIA MGAYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya GUTA yenye usajili namba MC 224 CSS.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **NJ/TR/RB/393/2023**



**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA BUKOBA**
**RUFAA YA MADAI NA. 5/2023**
**LAURENT DAUD.......................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**BISHOP BAYONA MUTASHOBYA.........MJIBU RUFAA WA KWANZA**
**CRIAN PANTALEO.................MJIBU RUFAA WA PILI**

**WITO/ KUITWA SHAURINI.**

**Kwa BISHOP BAYONA MUTASHOBYA POPOTE ULIPO**

Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la Rufaa tajwa juu imepangwa kusikilizwa tarehe 16 mwezi Agosti mwaka 2023 saa 8:30 mchana, mbele ya Mh. I. K. BANZI, JAJI wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako, shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 17 mwezi Julai mwaka 2023.



**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**BUKOBA**

## HABARI KITAIFA

MIFUGO HIFADHINI

# Korti Kuu yaamuru waliopigwa faini warudishiwe fedha zao

**Na Tumaini Mafie,**
ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha imetoa hukumu ya kesi Na. 9 ya 2023 ya kupinga faini ya Sh. 100,000 kwa kila ng'ombe aliyeingizwa katika pori la akiba na kuamuru walalamikaji kurudishiwa Sh. milioni tatu kama fidia kwa kuwa kiasi hicho hakikuwa halali kutozwa.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Mohamed Gwae, alisema Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009 inaelekeza faini ya mifugo kuingia katika pori la akiba ni Sh. 200,000 na haitakiwi kuzidi Sh. milioni 10.

Alisema siyo sahihi kutoza faini kulingana na idadi ya mifugo, bali ilihitajika kutoza faini kutokana na kosa la mifugo kuingia katika Pori la Akiba la Pololeti.


Katika kesi hiyo, waombaji rufani walidai kulipishwa Sh. 100,000 kwa kila ng'ombe na Sh. 25,000 kwa mbuzi, hivyo walizazimika kulipa jumla ya Sh. milioni 13 kwa faini ya ng'ombe na Sh. milioni 2.5 kwa faini ya mbuzi.

Katika kesi hiyo waleta maombi waliwakilishwa na Mawakili Joseph Oleshangay na Denis Moses huku upande wa wajibu rufani ukiwa ni Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mkurugenzi wa Wanyamapori na Jamhuri.

Nje ya mahakama, waombaji rufani walishukuru mahakama kwa kutoa ufafanuzi wa kisheria na kutoa amri warudishiwe fedha zao.

"Tunaishukuru mahakama na mawakili wetu kwa namna ambavyo wamepambania hii kesi na hatimaye leo tumepata suluhisho la sisi kulipwa fedha zetu maana tulilazimika kulipa ili mifugo yetu isipotezwe au kuteseka na njaa," alisema Raphael Oleruye.

Waombaji rufani katika kesi hiyo ni Raphael Oleruye na Baraka Kimoson kutoka Nainokanoka, Ngorongoro, mkoani Arusha.




Gavana wa Benki Kuu (BoT), Emmanuel Tutuba (mwenye miwani katikati), akiangalia jinsi ya kuskani kinywaji kwa mfumo wa kielektroniki (ETS) unaotolewa na kampuni ya SICPA ili kuhakiki stempu za kinywaji, katika banda la Mamlaka ya Mapato (TRA) jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi TRA, Richard Kayombo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Bila maoni ya wananchi hakuna utawala bora'

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

MKURUGENZI wa Kituo cha Taarifa kwa Wananchi (TCIB), Deus Kibamba, amesema dhana ya uongozi bora haiwezi kuzungumziwa ikiwa mipango ya serikali haina maoni ya wananchi.

Vilevile, ameitaka serikali kukerwa inapoona wananchi hawana taarifa kuhusu mambo mbalimbali yanayotekelezwa ikiwamo bajeti ya serikali.

Kibamba alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipotoa mada katika Jukwaa la Ufahamu lililofanyika mjini Kibaha, likiandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Vijana la Youth Partnership Countrywide (YPC). Alisema serikali inatakiwa kufurahia wananchi kuwa na taarifa ya kila jambo, ikiwamo miradi ya miradi inayojengwa pamoja na utekelezaji wa bajeti iliyopangwa, wananchi wanapaswa kufahamu kila hatua.

"Lazima wananchi wawe na taarifa ya bajeti na vyanzo vyake kutokana na hivyo wanaweza kufuatilia bajeti iliyopita kabla ya mchakato wa bajeti mpya. Ikitokea hawajashirikishwa, basi kinachotekelezwa hakitokani na wananchi," alifafanua.

Kibamba pia aliwakumbusha wananchi kushiriki katika mikutano kupata taarifa mbalimbali, pia kujenga utaratibu wa kufuatilia miradi na kusoma ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mkurugenzi wa YPC, Israel Ilunde alisema jukwaa hilo linafanyika kila mwezi na mada mbalimbali zinatolewa kwa lengo la kuwapa elimu wananchi na kuwahamasisha kushiriki mikutano kuanzia ngazi ya mitaa na kufuatilia na kulinda miradi inayotekelezwa. Mmoja wa washiriki wa jukwaa hilo, Monica Simon, alisema mada zinazotolewa zinawajenga na kuwafungua ufahamu kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali na pia kuwa washiriki katika uandaaji wa bajeti kwa kuweka vipaumbele katika maeneo yao.


## MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF)

We Build Your Future

## MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii utauza kwa njia ya Mnada wa Hadhara Magari chakavu katika Mikoa ya **Dar es salaam, Pwani, Kilimanjaro, Mtwara, Kagera, Morogoro na Songwe** katika vituo na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini.

**1. MKOA WA DAR ES SALAAM**

| TAREHE | KITUO | AINA YA MAGARI YATAKAYOUZWA |
|---|---|---|
| 15 AGOSTI 2023 | NSSF ILALA | TOYOTA LANDCRUISER GX V8, NISSAN CIVILIAN COASTER, TOYOTA LANDCRUISER GX V8, NISSAN PATROL, TOYOTA LANDCRUISER STANDARD, TOYOTA LANDCRUISER STANDARD, TOTOTA LANDCRUISER STANDARD, TOYOTA LANDCRUISER GX V8, TOYOTA RAV4, TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP, TOYOTA LANDCRUISER STANDARD, TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP |
| 16 AGOSTI 2023 | NSSF MIKOCHENI | TOYOTA LANDCRUISER GX V8 |
| | NSSF TABATA FLATS (AROMA) | ISUZU PSR WATER BOWSER |

**2. MKOA WA PWANI**

| TAREHE | KITUO | AINA YA GARI LITAKALOUZWA |
|---|---|---|
| 18 AGOSTI 2023 | NSSF PWANI (KIBAHA) | TOYOTA LANDCRUISER GX STANDARD |

**3. MKOA WA MTWARA**

| TAREHE | KITUO | AINA YA GARI LITAKALOUZWA |
|---|---|---|
| 21 AGOSTI 2023 | NSSF MTWARA | NISSAN PATROL |

**4. MKOA WA KAGERA**

| TAREHE | KITUO | AINA YA GARI LITAKALOUZWA |
|---|---|---|
| 25 AGOSTI 2023 | NSSF KAGERA | NISSAN PATROL |

**5. MKOA WA KILIMANJARO**

| TAREHE | KITUO | AINA YA GARI LITAKALOUZWA |
|---|---|---|
| 29 AGOSTI 2023 | NSSF KILIMANJARO | TOYOTA LANDCRUISER STANDARD |

**6. MKOA WA MOROGORO**

| TAREHE | KITUO | AINA YA GARI LITAKALOUZWA |
|---|---|---|
| 02 SEPTEMBA 2023 | NSSF MOROGORO | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP, LANDROVER DEFENDER 110 |

**7. MKOA WA SONGWE**

| TAREHE | KITUO | AINA YA GARI LITAKALOUZWA |
|---|---|---|
| 05 SEPTEMBA 2023 | NSSF SONGWE | TOYOTA LANDCRUISER STANDARD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya Chombo/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa Chombo/kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
4. Ruhusa ya kuangalia vyombo itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada husika;
6. Mnada utaanza saa Nne (04:00) asubuhi katika kila kituo.

**MKURUGENZI MKUU**

217524001

MAKALA MAALUM

## MHARIRI AKIRI:

# Tuzo ya EJAT imeniongezea thamani

**SANULA Athanas, Mhariri Msanifu wa gazeti la Nipashe, aliyepata Tuzo ya EJAT ya Umahiri wa Uandishi wa Habari, alipokutana na Ndimara Tegambwage, mshindi wa Tuzo ya Mafanikio katika Maisha ya Uandishi wa Habari (2022). Soma nukuu...**



Mgeni Rasmi wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2022, Balozi Ombeni Sefue, akikabidhi tuzo ya Mshindi wa Jumla kwa Mhariri Msanifu wa gazeti la Nipashe, Sanula Athanas, mkoani Dar es Salaam Julai 22 mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Ndimara:** Tuzo hii ya Umahiri wa Uandishi wa Habari ya EJAT uliyopata juzi (22/7/2023), ina maana gani kwako leo?

**Sanula:** Ni tuzo iliyothibitisha kile nilichokiamini tangu nikiwa kijana wa miaka 19 mwaka 2006 kwamba mimi ni "mtu." Nitakuja kufanya jambo ambalo litapendwa kitaifa na ikiwezekana kimataifa. Leo, hii ni tuzo inayonitambulisha zaidi kwamba kuna mwandishi wa habari anaitwa Sanula. Wale ambao hawakuwa wananijua vizuri, bila shaka wamehangaika kupekua huku na kule kusaka taarifa juu yangu.

Hii ni tuzo ambayo imeongeza thamani yangu. Sasa si Sanula tu, bali Mwandishi Bora kwa mwaka 2022 katika tuzo za kitaifa.

**Ndimara:** Unatarajia tuzo hii ikuongezee nini katika uandishi wako wa habari?

**Sanula:** Tuzo imenipa nguvu ya kuandaa kazi bora zaidi. Imetoa heshima kwa kazi nzuri ninazozifanya kuwezesha jamii kutatua matatizo yanayoikabili. Ni kengele kwangu kwamba kumbe ukiandaa kazi bora, zinalipa! Ninapaswa kuongeza ubora zaidi katika kazi zangu.

Kazi zilizonipa ushindi, zilikuwa zimekamilika - nilifunua tatizo, nikalianika, wanaohusika wakazinduka, wakafuatilia, wakatekeleza na jamii ikapata furaha. Nilifuatilia utekelezaji wake katika kulitatua - mwanzo hadi mwisho.

**Ndimara:** Hii si mara ya kwanza kwako kupata tuzo ya EJAT. Tuzo ya kwanza ilikuwa "bwana mdogo" kwa hii ya juzi. Ina maana ulijiapiza kupata Tuzo ya juu?

**Sanula:** Ni kweli! Kabla ya tuzo tatu nilizotunukiwa mfululizo juzi (Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Elimu 2022, Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Utalii na Uhifadhi 2022, na Tuzo ya Mshindi wa Jumla EJAT 2022); nilikuwa nimeshapata tuzo 16 za EJAT (11 za mshindi wa kwanza katika kategoria nilimoandika na tano za nafasi ya pili na ya tatu). Ni mwaka wa tatu sasa mfululizo ninaingia fainali ya kumpata Mshindi wa Jumla wa EJAT - 2020, 2021 na 2022. Nilipokosa tuzo hiyo ya juu mwaka 2020, nilijiapiza kulisaka taji kwa kuandaa kazi kwa ubora zaidi. Imetimia!

**Ndimara:** Una mradi wa kukusanya tuzo kila mwaka?

**Sanula:** Ndiyo. Ninapenda kushindanisha kazi zangu ili kupima ubora. Kwa Tanzania kuna tuzo nyingi kwa ajili ya waandishi wa habari, lakini huwa sishiriki mashindano hayo; mimi niko EJAT. Tuzo zingine nyingi hapa nchini zinaandaliwa kwa kuzingatia vigezo vinavyowapendeza waandaaji wa tuzo - si vigezo vya kitaaluma katika uandishi wa habari. EJAT ni sehemu sahihi ya kupima uwezo na mafanikio ya mwandishi wa habari.

**Ndimara:** Kampuni unakofanya kazi inakuchukulia kuwa mwandishi wa habari wa aina gani ukizingatia tuzo hizi?

**Sanula:** Ofisini wananichukulia kama mwandishi wa habari za uchunguzi na uwajibikaji; mwalimu kwa waandishi vijana na mwandishi mwenye tuzo nyingi zaidi katika historia ya EJAT.

**Ndimara:** Wewe unaandika kwa kushindana au tuzo ndizo zinakufuata?

**Sanula:** Kama nilivyodokeza awali. Ninapenda kushindanisha kazi zangu ili kupima ubora wa kazi ninazoandaa; lakini siandiki kwa lengo la kushindana. Lengo langu la kwanza ni kuchochea uwajibikaji ili kuleta ustawi wa jamii kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuzo zinakuja kutokana na kuandaa, kuandika na kuchapisha kazi bora zenye mguso kwa jamii na zinazozingatia misingi ya taaluma ya uandishi wa habari.

**Ndimara:** Kuna mashindano mbalimbali ya uandishi bora katika nchi nyingi za Afrika na duniani. Umewahi kushindanisha kazi zako huko; matokeo yake yalikuwaje?

**Sanula:** Katika miaka yangu 11 ya uandishi wa habari, sijawahi kushiriki shindano lingine la uandishi wa habari mbali na EJAT. Ninatarajia kushiriki mashindano ya Tuzo za SADC kuanzia mwaka huu.

**Ndimara:** Una cha kusema juu ya Baraza la Habari Tanzania (Media Council of Tanzania - MCT) katika uendeshaji mashindano haya ya EJAT kila mwaka?

**Sanula:** MCT wanastahili pongezi kwa kuandaa tuzo hizi kila mwaka licha ya kuwapo vikwazo katika miaka ya karibuni; kwa mfano, kuyumba kiuchumi kwa baadhi ya taasisi zinazowafadhili - kipindi cha mlipuko wa UVIKO-19.

Ninafikiri kuna haja kupata wafadhili zaidi ili kuchochea ushiriki mpana wa waandishi wa habari; na kuinua vipaji vingi vinavyopigania weledi katika taaluma hii.

Pia ninawapongeza MCT kwa uwazi katika kuwapata washindi. Sijawahi kuona upendeleo. Kazi bora ndiyo inashinda.

**Ndimara:** Unasema hivyo kwa kuwa una rekodi ya kushinda mara nyingi au unaona kazi zako ni bora kweli kuliko za wengine?

**Sanula:** Kwa miaka mitatu iliyopita, niliandaa kazi zenye ubora na zilizochochea uwajibikaji serikalini na katika jamii. Ni kazi hizi zilizonifikisha hatua ya kuingia fainali tatu za kumsaka Mshindi wa Jumla wa EJAT 2020, 2021 na 2022.

Nimeshiriki mashindano haya kwa miaka 11 mfululizo. Mwaka 2013 niliangukа. Kazi yangu niliyowasilisha kwa majaji - kipindi hicho nikiwa mwandishi wa habari za michezo - ilitupwa. Sikulalamika. Nilipoingalia kwa vigezo, nikakiri moyoni kwamba sikustahili.

Mwaka 2017 pia nilikumbana na ushindani mkali. Nikaanguka. Nikaangalia kazi ile pia kwa vigezo. Nikakubali kushindwa.

Kwahiyo, kwa uzoefu wangu wa zaidi ya miaka 10, nikiwasilisha kazi zangu kwa kamati ya EJAT, nimeona hakuna upendeleo wala uonevu kwa washiriki. Ukipita, furahi na jiandae kusonga mbele. Ukikwama, usikate tamaa. Jitathimini ulikoanguka. Jipange kuleta kazi mpya, bora na shindanishi.




**2021:** Mwandishi Bora wa Habari za: Haki za Binadamu; Habari za Sayansi na Teknolojia.



**2014:** Mwandishi Bora wa Habari za Michezo na Utamaduni.



**2015:** Mwandishi Bora wa Habari za Michezo na Utamaduni.



**2016:** Mwandishi Bora wa Habari za Kodi na Ukusanyaji Mapato.



**2018:** Mwandishi Bora wa Habari za Uchumi, Biashara na Fedha.



**2019:** Mwandishi Bora wa Habari za: Haki za Binadamu na Utawala Bora; Habari za Utalii na uhifadhi.

TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.06.2023

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Jun-23 | Robo Mwaka ya 31-Mar-23 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,904 | 4,114 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,120 | 12,889 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 88,392 | 87,794 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | - | 6,321 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 1 | 4 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | 5,508 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 73,698 | 60,119 |
| 12 | Mali Nyingine | 118,356 | 91,375 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 5,159 | 2,912 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **306,630** | **271,035** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 64,965 | 48,685 |
| 18 | Amana za Wateja | 195,774 | 180,314 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 7,941 | 5,312 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,239 | 1,408 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,781 | 3,477 |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,453 | 4,655 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **277,153** | **243,851** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** !"#$%&'()$*+, | **29,477** | **27,185** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (39,925) | (39,754) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,780 | 1,318 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 5,097 | 5,097 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **29,477** | **27,185** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 613,257 | 595,247 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 9,060 | 9,404 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 5,622 | 5,412 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10% | 10% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 14% | 15% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 39% | 33% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 24% | 22% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85% | 88% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 10% | 23% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 13% | 16% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-23 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 5,133 | 3,592 | 9,311 | 7,160 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,429) | (1,157) | (2,775) | (2,220) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **3,704** | **2,435** | **6,537** | **4,940** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | | | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (211) | - | (257) | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **3,804** | **2,806** | **6,548** | **5,324** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,974 | 450 | 2,849 | 864 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,809 | 2,350 | 3,645 | 4,430 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 22 | 6 | 55 | 30 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(4,752)** | **(4,205)** | **(8,883)** | **(8,492)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,047) | (1,792) | (4,065) | (3,761) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (556) | (383) | (840) | (775) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (2,150) | (2,030) | (3,978) | (3,956) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **2,545** | **1,036** | **3,945** | **1,772** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (82) | (113) | (165) | (150) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,463** | **923** | **3,780** | **1,622** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **2,463** | **923** | **3,780** | **1,622** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 141.00 | 127.00 | 141.00 | 127.00 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 391.92 | 146.82 | 601.58 | 258.10 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 8.00 | 7.00 | 8.00 | 7.00 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 3.52% | 0.53% | 2.73% | 0.92% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 34.77% | 3.63% | 26.69% | 6.38% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 53.17% | 65.73% | 56.01% | 68.03% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 9.39% | 2.06% | 8.29% | 4.18% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Jun-23 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Mar-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **2,463** | **1,318** | **3,780** | **1,622** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 752 | 252 | 1,004 | 557 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (12,559) | 6,696 | (5,862) | 2,207 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 34,369 | 35,198 | 69,568 | (2,438) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (599) | (35,296) | (35,894) | 9,392 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (201) | (427) | (629) | 732 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (27,059) | (4,541) | (31,601) | 11,480 |
| - Kodi Iliyolipwa | (82) | (392) | (475) | (37) |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(2,915)** | **2,807** | **(108)** | **23,515** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (174) | (262) | (436) | (4,201) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(174)** | **(262)** | **(436)** | **(4,201)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - | - | - |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(3,090)** | **1,352** | **(1,738)** | **1,942** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 24,113 | 22,762 | 46,875 | 47,685 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **21,024** | **24,113** | **45,137** | **49,627** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2023
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2023** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,925) | 5,097 | - | - | 25,696 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 3,780 | - | - | - | 3,780 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(36,145)** | **5,097** | **-** | **-** | **29,477** |
| **Mwaka uliopita 2022** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (36,525) | 487 | - | - | 24,486 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,210 | - | - | - | 1,210 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | (4,610) | 4,610 | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(39,925)** | **5,097** | **-** | **-** | **25,696** |

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Gbenga Makinde<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | Imesainiwa | 26 Julai 2023 |
| 2 | Benson Msangi<br>**Afisa Mkuu wa Fedha** | Imesainiwa | 26 Julai 2023 |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | Imesainiwa | 26 Julai 2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | 26 Julai 2023 |
| 2 | Ebele Ogbue<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | 26 Julai 2023 |

United bank of Africa (T) Ltds is a subsidiary of United Bank of Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa, USA, Europe & UAE.

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana
- Benin
- Burkina Faso
- Cote D'Ivore (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

**United Arab Emirates**
- Dubai

217527402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati sasa kwa kila Klabu Ligi Kuu kuwa na timu za wanawake

**KUANZIA** msimu huu kanuni mpya ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), inazitaka klabu zote zitakazoshiriki michuano yake; Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho kuwa na timu za wanawake.

Hilo halikuzishtua Klabu za Simba na Yanga ambazo tayari zina timu za wanawake, Simba Queens na Yanga Princess zinazoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake nchini na mashindano mengine ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, kazi kubwa ilikuwa kwa timu za Azam FC na Singida Big Stars (Singida Fountain Gate) ambazo zilikata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa msimu ujao wa mashindano hayo unaoanza Agosti 18, mwaka huu. Katika kukidhi vigezo, Azam FC ikalazimika kuingia ubia na klabu ya Baobab ya Dodoma ambayo itatumika kama ndiyo timu ya wanawake ya Azam, huku kukawa na makubaliano ya baadhi ya viongozi wa Fountain Gate kununua hisa Klabu ya Singida Big Stars na kuifanya kubadilisha jina kuwa Singida Fountain Gate FC.

Klabu ya Fountain Gate ina timu ya mpira wa miguu ya wanawake inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake nchini, hivyo tunaweza kusema lengo la mchakato mzima ni kuifanya tu Singida Big Stars iwe na timu ya soka ya wanawake na kukidhi vigezo vilivyowekwa na CAF.

Hata hivyo, pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, nchini (TPLB), Almasi Kasongo, kusema bado kuna tatizo la viwanja, utawala, ofisi za klabu, fedha na eneo la soka la vijana ili klabu ziweze kufuzu kuwa na kanuni za leseni za Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini hili la kuwa na timu za wanawake sasa linapaswa kupewa kipaumbele.

Ni kweli kabisa tutamuunga mkono Ofisa Mtendaji Mkuu huyo wa Bodi ya Ligi, lakini bado kuna lingine tunamwongezea kuwa na timu za mpira wa miguu wanawake kufanywa kuwa lazima. Kama tayari CAF imeshaanza kuweka kanuni ya kuwa timu inayokata tiketi ya kucheza mechi za kimataifa ni lazima iwe na timu ya soka wanawake ama kuingia ubia wa uendeshaji wa timu hiyo na nyingine, basi hilo pia linafaa lianze kuangaliwa kwa macho matatu kwani tuendapo ipo siku hata kipengele hicho cha kuingia ubia kitafutwa hivyo klabu zetu kujikuta zikipoteza nafasi hiyo ya kuiwakilisha nchi kimataifa.

Tunakumbuka wakati wa mchakato wa Azam na Singida Big Stars kusaka timu za wanawake, Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Salum Madadi, aligusia kuwa kama ni hivyo basi itabidi nao misimu kadhaa mbele wafikirie kuweka kanuni hiyo na si tu ili kuinua soka la wanawake pekee bali kuzirahisishia kazi timu zitakazofuzu kimataifa.


Kwa sasa ukiacha timu nne zinazocheza michuano ya kimataifa, timu ambazo zinaweza zikapata nafasi ya kucheza michuano hiyo ya CAF na kukidhi vigezo hivyo ni Geita Gold na JKT Tanzania.

Timu ya Geita Gold wanawake imepanda Ligi Kuu msimu huu na JKT Queens ndiyo Mabingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa maana hiyo ni wakati sasa kwa Bodi ya Ligi kuanzisha mchakato pia wa timu za Ligi Kuu kuwa na timu za wanawake.

Inaweza kuweka kanuni kuwa timu yoyote kutoka chini, ikipanda tu Ligi Kuu ili iruhusiwe kucheza iwe na timu ya soka ya wanawake inayoshiriki hata Ligi daraja la pili ama la tatu.

Nipashe tunaamini wakati ni huu sasa kwa Shirikisho la Soka nchini na TPLB kuweka kanuni hiyo kwa klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu kuwa na timu za wanawake, jambo ambalo litachangia sana kuibua vipaji zaidi mikoani kwa jinsia hiyo tofauti na ilivyo kwa sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Mandonga ashauriwe kuacha kutopigana kama mechi za ligi

Na Adam Fungamwango

**BONDIA** Karim Mandonga alipigwa katika raundi ya tatu na sekunde 20 kwenye pambano la masumbwi lililofanyika jijini Mwanza usiku wa Jumamosi, Julai 29.

Ilikuwa ni siku nne tu baada ya kutoka nchini Kenya kucheza pambano lingine dhidi ya Daniel Wanyonyi ambalo alipigwa kwa pointi.

Binafsi, nilipositia Mandonga anacheza Jumamosi usiku dhidi ya Moses Gulola, tena ikiwa ni siku nne baada ya kutoka kucheza pambano lingine Julai 25, mwaka huu, nchini Kenya ambalo alimaliza zote 10, nilijua haweza kushinda.

Na kweli ndivyo ilivyotokea na kwa siku za karibuni kwa jinsi alivyoboresha kiwango chake, ilikuwa si rahisi kumpiga Mandonga kwenye raundi ya tatu tu.

Amepigwa kutokana na uchovu, labda na maumivu ambayo bado alikuwa nayo baada ya mechi dhidi ya Wanyonyi.

Inawezekana pia kama asingecheza pambano dhidi ya Wanyonyi angeweza kushinda.

Lakini mimi sitaki kwenda huko kwenye kushinda kwa sababu Mandonga yeye kushinda kwake wala si tatizo, haimpi tabu na mashabiki wake wanafurahi zaidi apigwe kuliko anaposhinda.

Mashabiki wa Mandonga wanampenda kutokana na tambo zake, ucheshi, mbwembwe, mikwara, lakini yote hiyo huwa anaishia kupigwa, wao ndiyo furaha yao.

Kwa miezi kadhaa hivi karibuni amekuwa akishinda mapambano yake mengi ya ndani na nje, pamoja na kwamba ilikuwa inawapa faraja sana mashabiki wake, lakini haiwapi furaha. Akipigwa au kupoteza pambano ndiyo furaha yake.

Hata mwenyewe huwa halalamikii maamuzi anapopigwa, ila huwa hakubali na anaomba tena mechi ya marudiano.

Ana kaulimbiu yake anayosema akipiga kama amepigwa na akipigwa kama amepiga. Sababu ni ile ile, mashabiki wake hupata faraja akipiga, lakini hufurahi anapopigwa.

Waandaaji nao wamekuwa wakimtumia kama kivutio katika biashara yao kwenye ngumi kwani ametokea kuwa kivutio kikubwa kwenye tasnia hiyo ya ngumi.

Kwenye mlolongo wa mabondia watakaopigana bila Mandonga huonekana kama halitokamilika na halitovutia pia.

Hapo ndipo umuhimu wa bondia huyo huonekana na kutafutwa, kusainishwa mkataba ili akapigane. Si vibaya kwa sababu ndiyo sehemu yake sasa ya kutafutia riziki, na kipindi hiki ambacho amekuwa maarufu anapaswa akitumie vizuri kwa sababu ustaa huwa unaisha pia.

Lakini anapaswa kuwa makini kwani anahatarisha afya na maisha yake kwa kupigana mfululizo. Ni hatari mno kwa mchezo wa ngumi kupigana kwa siku chache zinazotofautiana kama za mechi za mpira wa miguu mfano wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ilikuwa ni kama tu timu ya mpira wa miguu imecheza nchini Kenya siku ya Jumanne na Jumamosi ikacheza mechi nyingine Tanzania.

Hata kocha wa timu ya soka anaweza kusema timu yake ilikuwa na uchovu wa mechi na kusafiri pia, sasa fikiria mtu aliyepigana kwa raundi 10.

Mandonga anapendwa sana, lakini ili kuendelea kumsapoti inatakiwa ashauriwe asipigane ngumi mfululizo badala yake akae japo miezi mitatu kama inavyoshauriwa na wataalamu wa masumbwi kabla ya kupigana tena.

Ngumi ni mchezaji hatari unaoweza kusababisha ulemavu, afya ya akili na hata kifo kama yeye mwenyewe au wahusika katika usimamizi wa ngumu watamuacha aendelee kucheza masumbwi mfululizo.

Ili kuendelea kumuona, Mandonga akiburudisha, kumshangilia na yeye mwenyewe kupiga pesa kutokana na mchezo huo, anatakiwa atengenezewe mazingira ya kumlinda afya yake, vinginevyo tunaweza kumpoteza hata kwa kushindwa kupigana kutokana na afya kutomruhusu kwa tabia ya kupigana kila baada ya muda mfupi.

# TEF: Leseni ya magazeti iwe miaka 15

**Na Joseph Mwendapole**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa habari wameiomba serikali kurefusha muda wa uhai wa leseni ya usajili wa magazeti hadi kufikia miaka 15 badala ya mwaka mmoja wa sasa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Deodatus Balile, wakati wa mafunzo ya siku mbili kwa wahariri kuhusu Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari (MSA).

Alisema usajili wa magazeti, viwango vya elimu kwa waandishi wa habari na muda wa leseni za magazeti viko kwenye kanuni kwa hiyo wadau watakwenda kuzungumza na serikali kuweka kanuni ambazo hazitawaumiza wamiliki wa vyombo vya habari.

"Sasa tunakwenda kuzungumza na serikali ili kuandika kanuni tuangalie je magazeti yatasajiliwa kwa mwaka mmoja, miaka mitano, 10 au 15, redio za jamii zinapewa leseni ya miaka mitano, televisheni na redio zinapewa leseni ya miaka mitano, kwa hiyo tutajadiliana na serikali ili iweke kanuni nzuri," alisema.

Aidha, Balilie alisema kampuni za simu zinapewa leseni ya miaka 25 na kwamba lazima wadau waiombe serikali iongeze muda wa leseni za usajili wa magazeti kufikia angalau miaka 15 badala ya kusajiliwa kila mwaka.

Pia, serikali kurefusha uhai wa matumizi ya vitambulisho vya waandishi wa habari (Press cards) ambavyo kwa sasa wanalazimika kuomba kila mwaka.

"Hati ya kusafiria inatolewa kwa miaka 10, Press Card inaweza kutolewa kwa muda mrefu zaidi, leseni ya magazeti nayo inaweza kutolewa kwa muda mrefu zaidi badala ya kila mwaka na kwenye majadiliano sisi wadau tunakwenda tukiomba leseni ya magazeti iwe miaka 15 na serikali itakuja na hoja zake tutajadiliana tufikie mwafaka kwa mustakabali wa taifa letu," alisema.

Alisema wadau wa vyombo vya habari wamefurahi kuona kwenye mabadiliko ya sheria hiyo kifungu cha 50 (i) kimefanyiwa marekebisho na kuondoa dhana ya kashfa kuwa jinai na badala yake kuwa madai baina ya watu wawili wanaotuhumiana.

"Leo hii mtu akiniita mbwa mimi ndiye nitakayekwenda mahakamani kudai kwamba huyu mtu amenikashfu, lakini kabla ya mabadiliko haya mtu akimsema kiongozi wa serikali, polisi walikuwa wanamkamata huyo mtu na kumshtaki kwamba amemkashifu kiongozi wa serikali," alisema.

"Kwa sasa polisi wanaweza kukamata mtu na kumshtaki kwenye makosa ya jinai tu mfano mtu akinipiga kibao au akampiga mtu yeyote atashtakiwa kwa jinai kwasababu ni kosa la jinai lakini mtu akisema mtu fulani ni mwongo au ni mwizi anayetuhumiwa ndiye anawajibika kwenda mahakamani kumshtaki aliyemwita mwizi au muongo," alisema.

Alisema kifungu cha 53 kimefuta mamlaka ya mahakama kutaifisha mitambo iliyodaiwa kuchapisha makosa ya jinai, lakini kifungu cha (iV) kinachompa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Maelezo kutoa leseni, kusitisha leseni na kukataa kutoa leseni bado kipo.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo ambaye ni Mhadhiri wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC), Dk. Darius Mukiza, alisema uandishi ni taaluma kama zingine na siyo kazi ambayo inaweza kufanywa na mtu yeyote ambaye hana utaalamu hiyo.

"Sheria ilipitishwa na Bunge inasema angalau mwandishi awe na stashahada hii ni dhana ya kuifanya taaluma hii iheshimike na napenda kuwaasa waandishi wenzangu na wale wanaofikiria kuwa waandishi wasifikieri ni kitu ambacho unaweza kuamka tu na kufanya kwa hiyo napendelea waandishi waongeze ujuzi kwenye fani," alisema.

"Hata kama una shahada elimu haina mwisho lazima ujiendeleze kwasababu mawasiliano yanabadilika kila siku na mwandishi mzuri ni yule anayeweza kufanya mambo mengi mwenyewe. Mtu huyo huyo anajua kupiga picha, kutumia mitandao ya kijamii, anajua kutumia drone sasa tukibweteka vyombo vyetu vitakosa maudhui ya kuwapa wasomaji," alisema Mukiza.

# Kiwanda kuipunguzia serikali gharama kuagiza mbolea nje

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imesema uzalishaji wa tani milioni 1.2 wa mbolea utakaofanywa na kiwanda cha Itracom, Nala jijini Dodoma, utaipunguzia gharama za kuagiza nje ya nchi na kushuka kwa bei ya pembejeo hiyo.

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA), Dk. Stephano Ngailo, alisema hayo wakati wa ziara ya kutembelea kiwanda hicho jana jijini hapa ili kuona uzalishaji wa bidhaa hiyo.

Alisema mahitaji ya mbolea nchini ni tani 600,500, lakini kiwanda hicho kinakwenda kuzalisha tani milioni 1.2, jambo ambalo litaondoa changamoto ya upatikanaji wa mbolea.

Alisema serikali inaagiza mbolea nje ya nchi, lakini hivi sasa tatizo hilo litakwisha.

TFRA pia, imewaagiza mawakala wa usambazaji mbolea nchini kuanza kusambaza mapema kwa wakulima ili kuepusha malalamiko ya upungufu wa bidhaa hiyo nchini.

Dk. Ngailo alisema mawakala wote waliosajiliwa na serikali kwa ajili ya usambazaji mbolea wanapaswa kuanza sasa kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

"Nawaagiza mawakala wote wanaotambulika na serikali kuanza sasa usambazaji wa mbolea kwa wakulima hatuhitaji kusikia malalamiko ya ucheleweshwaji wa mbolea kwa wakulima ili waendeshe kilimo chenye tija," alisema Dk. Ngailo.

Alisema msimu uliopita wamepokea malalamiko mengi ya wakulima kutofikiwa na mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali kwa ajili ya wakulima mbalimbali.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mbolea cha Itracom, Nduwimana Nazaire, alisema wataendelea kushirikiana na serikali ili kuhakikisha wanatekeleza matakwa ya nchi kwenye bidhaa ya mbolea.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MABADILIKO YA KIWANGO CHA USAJILI WA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)**

**1.0 Utangulizi**
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuufahamisha Umma kwa ujumla kuwa, Sheria ya Fedha, 2023 imefanya marekebisho ya kima cha usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kuongeza kima hicho kufikia shilingi milioni 200 kutoka kutoka kiwango awali cha shilingi milioni 100 kilichoanzishwa mwaka 2014. Utekelezaji wa hitaji hili umeanza tarehe 1 Julai 2023.

**2.0 Wajibu kwa Wafanyabiashara**
Ili kuwa na utekelezaji mzuri wa takwa hili la usajili, wafanyabiashara wanakumbushwa kuzingatia yafuatayo;

**a.** Walipakodi wote ambao wamepata mauzo ya shilingi milioni 200 kwa mwaka kwenye mauzo yanayotozwa kodi, wanapaswa kutuma maombi ya usajili wa VAT.

**b.** Kwa wafanyabiashara waliokwisha sajiliwa wenye mauzo chini ya shilingi millioni 200 kwa mwaka, watatakiwa kuomba kusitisha usajili wa VAT na kuwasilisha ritani ya mwisho ya VAT baada ya kufanya marekebisho kwa bidhaa za biashara walizo nazo mkononi wakati wa kusitishwa kwa usajili wa VAT kama inavyotakiwa na Kifungu cha 80 cha Sheria ya VAT, Sura 148. Baada ya kupokea barua ya kuthibitisha kusitishwa kwa usajili wa VAT kutoka TRA, mlipakodi anapaswa kurudisha cheti halisi cha usajili wa VAT kwenye ofisi ya TRA ya mkoa wa kikodi husika. Wakati wa utekelezaji wa zoezi hili, maofisa wa TRA watatembelea eneo la biashara husika ili kuhakiki bidhaa hizo.

TRA itaendelea kutoa elimu juu ya mabadiliko ya viwango vya usajili wa VAT kwa makundi mbalimbali ya walipakodi kwa ajili ya utekelezaji wa takwa hili la kisheria.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:-

| | |
|---|---|
| Tovuti | : **www.tra.go.tz** |
| Namba ya Bure | : **0800 110 016 au 0800 750 075 au 0800 780 078** |
| WhatsApp | : **0744 23 33 33** |
| Barua Pepe | : **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz** |

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Kidatah

A.J. Kidata
**Kamishna Mkuu**

217522302

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni | Aina ya Ombi la Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Sindano Traders Company Limited, S. L. P 472, Kahama. | Kiwanja Na. 12, Kitalu "H", Eneo la Kahama, Shinyanga. | Sindano William Machumu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 2. | Lina Lazaro Bamie, S.L.P 472, Kahama. | Kiwanja Na. 462, Kitalu "EE", Eneo la Shunu, Kahama, Shinyanga | Lina Lazaro Bamie (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 3. | Rubondo Holding Company Limited, S.L.P 453, Geita. | Eneo la Nyamalimbe, Geita. | Denis Simeon Masala (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Vilainishi | Ombi la Leseni Mpya |
| 4. | Petroafrica (T) Limited, S.L.P 4878, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 28, Kitalu "BIII", Eneo la Mkuyuni, Mwanza. | Yasin Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 5. | Hassani Hamis Nyamse, S.L.P 120, Magu. | Kiwanja Na.1, Kitalu "A", Eneo la Mikoroshini-Njiche, Kisesa Trading Centre, Magu, Mwanza | Hassani Hamis Nyamse (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 6. | Hass Petroleum (T) Limited, S.L.P. 78341, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.31, Kitalu "F", Eneo la Kasulu, Kigoma. | Abdulkadir Hussein (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 7. | Blue Wave Emporium Limited, S.L.P 11624, Mwanza. | Kiwanja Na. 147, Kitalu "AA", Eneo la Kiloleli, Busega, Simiyu | Ephrahim Stanley Fimbo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 8. | Seif Juma Seif, S.L.P 120, Magu. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Eneo la Bulila, Bukoba, Kagera. | Seif Juma Seif (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 9. | GM & Company (T) Limited, S.L.P 7788, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 112, Kitalu "1", Eneo la Viwanda Port Road, Mtwara. | Gabriel Michael Kessy (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 10. | Olympic Petroleum Msijute Mtwara, S.L.P 16484, Dar es salaam. | Kiwanja Na.94, Kitalu "A", Eneo la Msijute, Mtwara. | Ally Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 11. | Olympic Petroleum Mtwara, S.L.P 16484, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.1, Kitalu namba "A", Eneo la vigaeni, Mtwara. | Ally Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 12. | Manyunyu Traders Limited. S.L.P 860, Morogoro. | Kiwanja Na. 37, Kitalu "A", Eneo la Mwembesongo, Morogoro. | Focus Patrick (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa gesi ya kupikia | Ombi la Leseni Mpya |
| 13. | Laroil Tanzania Limited, S.L.P 15742, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 989, Kitalu "A", Eneo la Fire, Ilala, Dar es salaam. | Mohammed Hasham Lardhy (Mtanzania) | Leseni ya uuzaji wa jumla wa gesi ya kupikia (LPG) | Ombi la Leseni Mpya |
| 14. | Salima Oxygen Limited, S.L.P 19137, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "E", Eneo la Mbagala, Temeke, Dar es Salaam. | Mehboob Sumar. (Raia wa Kenya) | Leseni ya uuzaji wa jumla wa gesi ya kupikia (LPG) | Ombi la Leseni Mpya |
| 15. | R.K. Chudasama Limited S.L.P. 325 Dar es salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu '1', Eneo la Buguruni, Ilala, Dar es salaam. | Sundeep Vasantlal Chudasama (Mtanzania) | Leseni ya uuzaji wa jumla wa vilainishi | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 16. | Augusta Energy Tanzania Limited, S.L.P 1748, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 372, Kitalu '1' Eneo la Oyster pearl Galleria, Kinondoni, Dar es Salaam. | Orlando D'costa (Mtanzania) | Leseni ya Condensate | Ombi la Leseni Mpya |
| 17. | Tanzania International Petroleum Reserves Limited (TIPER), S.L.P 2608, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 01, Kitalu "01" Eneo la Vijibweni, Kigamboni, Dar es Salaam. | Mohammed Seif Mohammed (Mtanzania) | Leseni ya utunzanji wa mafuta. | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 18. | DMB Petroleum Limited, S.L.P 42445, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "B" Eneo la Chang'ombe, Temeke, Dar es Salaam. | Dahir Mbarak Salim (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 19. | Camel Gas (T) Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 365/366, Eneo la Kurasini, Temeke, Dar es Salaam. | Edha Abdallah Munif (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 20. | SRPG Energy Solution Limited, S.L.P 13356, Dar es salaam. | Kiwanja Na.22, Kitalu "B" Eneo la Kisutu, Ilala, Dar es Salaam. | Joshi Sachin (Raia wa India) | Leseni ya jumla ya mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 21. | Top Oil Petroleum Limited, S.L.P 42445, Dar es Salaam. | Eneo la Makondeko, Ubungo, Dar es salaam. | Mbaraka Bawazir. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 22. | Gulf Oil Co. Ltd - Tabata Mandela Service Station, S.L.P 105934, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 48, Eneo la Tabata, Ilala, Dar es Salaam. | Farid Abubakar. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 23. | Top Oil Petroleum Limited, S.L.P 42445, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 244, Kitalu "F", Eneo la Chamazi, Temeke, Dar es salaam. | Mbarak Bawazir. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 24. | Top Oil Petroleum Limited, S.L.P 42445, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2612, Kitalu "A", Eneo la Kitunda shule, Ilala, Dar es Salaam. | Mbarak Bawazir. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 25. | Puma Energy (T) Ltd, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 48/27, 62/27 & 47/66, Eneo la Upanga, Ilala, Dar es Salaam. | Fatma Mohamed Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 26. | Lake oil Buguruni Malapa, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 13/D, Eneo la Buguruni Malapa, Ilala, Dar es Salaam. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |
| 27. | Oiltech Filling Station, S.L.P 10, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "DD", Eneo la Kongowe, Kibaha, Pwani. | Joram Joshua Iranga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya. |
| 28. | Rashal Petroleum Limited, S.L.P 4660, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 16 & 17, Kitalu "E" Eneo la Nangando, Liwale, Lindi. | Farhiya Hersi Warsame (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni. |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

217528402

# TAARIFA YA VIWANGO VYA TIGO KUANZIA TAREHE 19 JULAI 2023

## Viwango unavyotozwa kwa kadri unavyotumia (Na Kodi)

**** - Malipo ya sauti yamekadiriwa kwenye sekunde iliyo karibu**
**- Malipo ya data yamekadiriwa kwa shilingi 0.09 kwa kila kilobaiti 10 za data**

**VIWANGO VYA NDANI**

| Aina za simu | Bei (TSh/Dk) |
|---|---|
| Tigo - Tigo (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |
| Tigo - Mitandao mingine (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA - TIGO**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 720 | China, India, Marekani, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Angola, Afrika Kusini, Nigeria, Botswana, Ghana, Ethiopia |
| Kundi 3 | 1020 | Lebanon, Israeli, Hispania, Falme za Kiarabu, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani) |
| Kundi 4 | 1200 | Sweden, Hong Kong, Pakistani, Yemen, Ufilipino, Saudi Arabia, Uholanzi, Japan, Malaysia, Norway, Ireland, |
| Kundi 5 | 1800 | Australia, Nepal, Uturuki, Urusi, Visiwa vya Comoro, Uganda, Rwanda, Ufaransa, Denmark, Italia, Oman, Ujerumani |
| Kundi 6 | 2520 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 7 | 2520 | Cuba, DRC, Burundi, Zimbabwe, Msumbiji, Uswisi, Malawi, Zambia |
| Kundi 8 | 19800 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA - ZANTEL**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 497 | Marekani, India, China, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Falme za Kiarabu, Afrika Kusini, Denmark, Sweden, Norway, Ireland, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani), Hispania, Ufaransa, Italia, Pakistan, Zimbabwe, Ujerumani |
| Kundi 3 | 1325 | DRC, Yemen, Omani, Lebanon, Israel, Sudani |
| Kundi 4 | 1500 | Zimbabwe (simu za kiganjani), Msumbiji, Malawi, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, Mayote, Sudani ya Kusini |
| Kundi 5 | 1200 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 6 | 3000 | Cuba, Vanuatu, Tunisia, Tonga (simu za kiganjani), Tokelau, Uswisi, Somalia,Visiwa vya Shelisheli, Nauru, Samoa, Madagascar, Slovenia, Visiwa vya Comoro |
| Special | 18000 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA SMS**

| Aina za SMS | Bei (TSh/SMS) |
|---|---|
| SMS za kitaifa | 8 |
| SMS za kimataifa | 215 |

**VIWANGO VYA DATA**

| Intaneti | Bei (TSh) |
|---|---|
| Data kwa MB | 9.35 |

## VIWANGO VYA VIFURUSHI VYA DAKIKA, INTANETI NA SMS (Na Kodi)

**MITANDAO YOTE**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 500 | 90 | 10 | 100 | 25 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 30 | 30 | 25 | 10 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 40 | 40 | 10 | 350 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 150 | 150 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 1500 | 0 | 180 | 180 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 1500 | 250 | 50 | 300 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 2000 | 0 | 250 | 250 | 100 | 50 | Siku 7 |
| 3000 | 0 | 450 | 450 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 3000 | 55 | 70 | 125 | 50 | 1024 | Siku 7 |
| 5000 | 100 | 180 | 280 | 100 | 1434 | Siku 7 |
| 5000 | 0 | 400 | 400 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 1200 | 1200 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 0 | 500 | 500 | 50 | 3072 | Siku 30 |
| 20000 | 0 | 800 | 800 | 50 | 7168 | Siku 30 |
| 30000 | 0 | 900 | 900 | 500 | 11264 | Siku 30 |

**SMS**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 200 | 0 | 0 | 0 | 200 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 0 | 0 | 0 | 1000 | 0 | Siku 7 |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 10000 | 0 | Siku 30 |

**BILA KIKOMO**

| Bei (TSh) | Dakika za Tigo-Tigo / Zantel-Zantel | Dakika za Mitandao yote | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1000 | 0 | 30 | 30 | 50 | 0 | Bila Kikomo |
| 1000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 250 | Bila Kikomo |

**INTANETI**

| Bei (TSh) | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | 246 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 492 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 985 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 950 | Siku 7 | N/A |
| 2100 | 1024 | Siku 7 | N/A |
| 3000 | 1434 | Siku 7 | N/A |
| 5000 | 2458 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 4920 | Siku 7 | N/A |
| 15000 | 7373 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 4920 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | 9830 | Siku 30 | N/A |
| 35000 | 17240 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | 24576 | Siku 30 | N/A |

**KIMATAIFA - TIGO**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 40 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Nigeria,Ghana - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Misri - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 4 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 80 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Nigeria,Ghana - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 6000 | Misri - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 5 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 12 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Nigeria,Ghana - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Misri - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | India, Marekani, Canada, China, Hong Kong - Dk 180 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Omani, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 18 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Ufaransa - Dk 13 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Kenya, Rwanda, Ethiopia - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Msumbiji, Angola, Botswana, Afrika Kusini - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Nigeria, Ghana - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Misri - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 24 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Oman, Falme za Kiarabu, Yemen, Pakistani, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 38 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Cameroon, Senegal, Ivory Coast - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Algeria, Morocco, Tunisia - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Zambia, Malawi, Zimbabwe - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Uganda, DRC, Burundi, Somalia - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |

**KIMATAIFA - ZANTEL**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | China, India - Dk 22 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 2500 | Oman - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ufaransa - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Afrika Kusini, Mauritius - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon, Yemen, Sudan, Misri - Dk 11 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Oman - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | China, India - Dk 110 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Ujerumani, Italia, Uingereza (simu za mezani), Uturuki - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 7500 | Kenya, Uganda, Rwanda - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |

** Mabadiliko haya yamehusisha pia vifurushi vya **SAIZI YAKO**

**MIC TANZANIA PLC,**
Derm Complex, Kiwanja Namba 11, Kitalu 45 A, Barabara ya Bagamoyo
S.L.P. 2929, Dar es Salaam, Tanzania.

**www.tigo.co.tz**

tigo

NIPASHE JUMATATU JULAI 31, 2023

Nipashe

Spotika



SABABU 5 KWA NINI MSIMU HUU WA EPL UTAKUWA MGUMU KWA ARSENAL UK. 12-13



OZIL

# WACHEZAJI WANNE WALIOUZWA MAPEMA ZAIDI REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

INAUMA sana mchezaji anapouzwa na klabu yako huku ukiamini angeweza kupata mafanikio makubwa zaidi, kama angepewa muda zaidi. Kwa upande wa Real Madrid, karibu kila mchezaji wanayemuuza anaonekana kama mauzo duni kwani lazima angekuwa mzuri sana baadaye.

Kwa klabu ambayo iko kileleni bila kuchoka, ni mara chache sana hakuna mtikisiko. Wachezaji huwa wanahamasishwa kwa sababu tu nafasi ya kuboreshwa imetokea katika soko la uhamisho. Real Madrid hawauzi wachezaji kwa faida, mauzo makubwa ya fedha huwa wakati fursa inapopatikana kutokana na klabu inayomnunua.

Wakati fulani, hata Real Madrid wanaweza kufanya makosa na biashara yao ya uhamisho. Wachezaji ambao walipaswa kuwashikilia kwa muda mrefu zaidi kuliko walivyofanya, na wachezaji ambao waliendelea kufurahia mafanikio ya ajabu mahali pengine.

Hapa tunawaangalia wachezaji wanne waliouzwa bila matarajio huku mashabiki wa Real Madrid wakibaki wakijiuliza 'itakuwaje'...

### Mesut Ozil: Mwaka 2013 kwenda Arsenal

Mesut Ozil aliishia kuwa na kazi isiyo ya kawaida. Alikuwa mwanasoka mwenye kipawa kikubwa aliyekuwa na mafanikio makubwa, lakini bado kuna hisia kwamba angeweza kufanikiwa zaidi. Mambo yalishuka kutoka kwa klabu na mtazamo wa kimataifa mwishoni mwa kukaa kwake Arsenal, lakini alikuwa mzuri zaidi Real Madrid.

Kulikuwa na uvumi kwamba ujio wa Luka Modric pale Madrid ulimfanya Ozil akose macho, lakini alikanusha na katika msimu wake wa mwisho akiwa na klabu hiyo, aliandikisha pasi nyingi za mabao kuliko mtu mwingine yeyote kwenye LaLiga. Huo ulikuwa msimu wa tatu mfululizo kuwa kiongozi wa pasi za mwisho kwenye LaLiga. Licha ya hayo, Real Madrid iliamua kukubali ofa ya pauni milioni 42.5 kutoka kwa Arsenal Septemba 2013.

Alifunga mabao 33 na asisti 59 katika mechi 184 za Ligi Kuu England na kusaidia Arsenal kutwaa Kombe la FA mara nne na Ngao ya Jamii moja. Kulingana na namba hizo na kile alichokifanya katika msimu wake wa mwisho Real Madrid, hakika bado alikuwa anahitajika kule Hispania.

### Angel Di Maria: Mwaka 2014 kwenda Manchester United

Kwa kiasi fulani sawa na hali ya Mesut Ozil, ilishangaza wengi kwamba Real Madrid walikuwa tayari kumnunua mwanasoka huyo mwenye kipaji cha ajabu. Inaonekana Di Maria alikuwa mwathirika wa ujio wa Gareth Bale na mwanzo mzuri aliokuwa nao mchezaji huyo wa Wales, huku Cristiano Ronaldo akiwa upande wa pili. Labda kama wangesubiri mwaka mmoja zaidi, Di Maria angechukua ulegevu ulioachwa na Bale.

Kupokea ada ya pauni milioni 59.7 kulionekana kuwa ofa nzuri sana kwa Real Madrid kukataa kutokana na kwamba Di Maria hakuonekana kama mchezaji anayeanza moja kwa moja, na huenda kucheza kwake Manchester United kuliwafanya wahisi kuwa wamethibitishwa. Alianza vizuri sana, lakini jeraha na maamuzi yasiyo ya kawaida kutoka kwa Louis van Gaal yalimaanisha kuwa United hawakumkaribisha Di Maria.

Alijiunga na PSG baada ya mwaka mmoja na alionesha kuwa bado ni mwanasoka mahiri, akicheza mara 295, akifunga mabao 93 na kutoa asisti 119 za ajabu. Ikizingatiwa jinsi muda wa Bale akiwa Real Madrid ulivyozidi kuzorota, kumbakisha Di Maria, mchezaji aliyetaka kubaki, lisingekuwa chaguo baya.

### Arjen Robben: Mwaka 2009 kwenda Bayern Munich

Bila shaka ni mfano bora, Arjen Robben alikuwa Real Madrid katika ubora wake, lakini si pale alipocheza soka lake bora zaidi. Winga huyo aliwasili baada ya kukaa Chelsea kwa miaka mitatu, lakini aliiongoza Real Madrid kwa misimu miwili pekee. Alikuwa mchezaji muhimu, akifunga mabao 13 na kupata asisti 15 katika mechi 65.

Ujio wa Florentino Perez kama rais wa klabu hiyo ghafla ulimpa presha Robben na wengine, kwani Cristiano Ronaldo na Kaka pia waliwasili. Licha ya ukweli kwamba Robben alikuwa akicheza vema na hakutaka kuondoka, alisafirishwa kwenda Bayern Munich ambao walipeleleza fursa ya kumsajili winga wa kiwango cha kimataifa kwa euro milioni 25 pekee.

Alishinda mataji 17 akiwa Bayern, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo alifunga bao la ushindi dhidi ya Borussia Dortmund. Alifunga mabao 144 na asisti 101 katika michezo 309, na Real Madrid wanaweza kuhisi wangeweza kupata zaidi kutokana na muda wake katika klabu, au angalau ada kubwa zaidi.

### Claude Makelele: Mwaka 2003 kwenda Chelsea

Sio tu kwamba Real Madrid walimwacha wazi Claude Makelele kuondoka katika klabu hiyo, kuna nukuu kutoka kwa Florentino Perez kuifanya kuwa mbaya zaidi. Baada ya kumwachia Makelele kuondoka mwaka 2003, Perez alisema: "Hatutammisi Makelele. Mbinu yake ni ya wastani, hana kasi na ustadi wa kuchukua mpira kuwapita wapinzani, na asilimia 90 ya usambazaji wake huenda nyuma au kando."

Baadaye aliongeza: "Wachezaji wadogo watakuja ambao watasababisha Makelele kusahaulika."

Makelele alikuwa ameomba kuongezewa mkataba mpya Real Madrid ikizingatiwa kuwa alikuwa analipwa mshahara wa chini lakini klabu ikakataa. Hiyo ilisababisha ombi la uhamisho. Steve McManaman alimuelezea Makelele kama kiungo muhimu zaidi, lakini asiyethaminiwa ndani ya Real Madrid katika wasifu wake.

Chelsea ilimnyakua Mfaransa huyo kwa pauni milioni 16, na akawa mchezaji muhimu. Aliisaidia Chelsea kushinda Ligi Kuu mara mbili, Kombe la FA mara moja, Kombe la Ligi mara mbili na Ngao ya Jamii. Alikuwa sehemu muhimu ya kuinuka kwa Chelsea hadi kuwa moja ya timu kuu za Ligi Kuu England.

## ISIKUPITE

BEKI wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Morocco, Nouhaila Benzina, ameweka historia kwa kuwa mchezaji wa kwanza kuvaa hijab kwenye michuano ya Kombe la Dunia. Uvaaji wa hijab kwa imani za kidini uliidhinishwa na Fifa mwaka 2014. Morocco ni moja kati ya timu nane zinazocheza kwa mara ya kwanza kwenye Kombe la Dunia la Wanawake msimu huu, ambapo Nouhaila alivaa hijab wakati wakishinda bao 1-0 dhidi ya Korea Kusini juzi.



# SABABU 5 KWA NINI MSIMU HUU WA EPL UTAKUWA MGUMU KWA ARSENAL

**LONDON,** England

ARSENAL iliwashangaza mashabiki na wachambuzi katika msimu wa 2022-23 wa Ligi Kuu England. Walitoa changamoto kubwa kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu na Manchester City.

**Baada ya kumaliza nafasi ya tano katika kampeni za awali, 'Washikabunduki' hao walikaa kileleni mwa msimamo wa ligi kwa siku 248 msimu uliopita.**

Huo ndio muda mrefu zaidi ambao timu imekaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England bila kutwaa ubingwa.

Arsenal wangetawazwa mabingwa wa England kama wangeweza kushinda mechi zao za mwisho.

Je, sasa wanaweza kuweka masikitiko yao nyuma yao na wachezaji wao kuendelea kutoa changamoto mpya kwa msimu mwingine?

Makala haya yanaangalia sababu tano kwa nini Arsenal wanaweza kuwa na wakati mgumu kwenye Ligi Kuu msimu ujao (2023-24).

### #Wapinzani watano bora wa EPL wameimarika zaidi

Manchester City ndio waliokuwa na uwezekano mkubwa wa kushinda taji la Ligi Kuu msimu uliopita. Hakuna timu nyingine ilionekana kuwa na nguvu kama wao kuelekea msimu huo. Ndio maana pia uthabiti na ubora wa Arsenal uliwashangaza wengi.

Liverpool hawakuimarika kama walivyohitaji msimu uliopita wa majira ya joto kabla ya msimu wa 2022-23. Tottenham Hotspur haikufanya kama ilivyotarajiwa. Newcastle United walikuwa waangalifu na wenye busara katika soko la uhamisho na walifanya kazi nzuri.

Manchester United walikuwa wakiendelea kujengwa upya na licha ya Erik ten Hag kufanya usajili wa kuvutia, mambo hayakutarajiwa kuwa sawa mara moja.

Chelsea walikusanya vipaji vingi ambavyo hawakuwa wamepanga kabisa mpango wao. Lakini hadithi imebadilika msimu huu wa majira ya joto na sita bora za Ligi Kuu zimefanya kazi nzuri kwenye dirisha la usajili, angalau kwenye karatasi.

Timu kama Liverpool, Chelsea, Manchester United na Newcastle United zimeimarika zaidi. Kwa hiyo, mambo hayatakuwa rahisi kwa Arsenal msimu huu.

### # Majukumu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya

Arsenal walikuwa wakicheza Europa League msimu uliopita. Walibakia kwenye kinyang'anyiro hicho hadi katikati ya Machi walipotolewa na Sporting Lisbon katika hatua ya 16-bora. Ligi ya Europa inafanyika Alhamisi na inafanya iwe vigumu kwa upande wowote kujipanga kabla ya mechi zao za ligi mwishoni mwa juma.

Kwa hiyo, Ligi ya Mabingwa Ulaya itakuwa rahisi zaidi kwenye miili ya wachezaji kwani michezo hii itafanyika Jumanne na Jumatano. Hata hivyo, kiwango cha ushindani katika Ligi ya Mabingwa ni cha juu zaidi. Kushinda Ligi ya Europa si kipaumbele kwa klabu za juu.

Kwa hiyo, makocha kwa kawaida walikuwa wakibadilisha wachezaji wao na kuwapa baadhi yao muda wa mapumziko Alhamisi usiku. Lakini hali hiyo ni tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa. Ni mashindano ya wakubwa. Washikabunduki hao watahitaji na kuangalia kuwa katika ubora wao mara mbili kwa wiki angalau hadi Krismasi.

Hilo linaweza kuchosha timu zaidi ya msimu uliopita na inaweza kusababisha viwango vyao vya uchezaji kushuka katika kipindi cha msimu huu.

### #3 Wanahitaji safu mpya ya ushambuliaji

Arsenal ilifunga mabao 88 kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, sita tu chini ya mabingwa Manchester City. Mabao yalitoka pande zote huku Gabriel Martinelli na Martin Odegaard wakifunga 15 kila mmoja huku Saka akifunga mara 14 kwenye ligi.

Mchezaji Gabriel Jesus alifunga mabao 11 huku akiuguza majeraha, Eddie Nketiah alifanya kazi nzuri. Folarin Balogun, ambaye alikuwa kwa mkopo kule Reims kwenye Ligue 1, alifunga mabao 21. Anaweza kuwa nyongeza nzuri kwenye safu ya Arsenal.

Hata hivyo, ripoti zinaeleza kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani anaweza kuwa njiani kuondoka katika klabu hiyo. Iwapo Balogun ataondoka, Arteta atabakia na Jesus na Nketiah kama chaguo zake mbili za kuvutia.

Ingawa wachezaji wote wawili wana sifa zao, si wafungaji mahiri.

### #2 Walipoteza ubora wao mwishoni

Arsenal walianza msimu wa 2022-23 kwa nguvu wakivuna ushindi mara kadhaa mfululizo na walikuwa wamekaa kileleni mwa jedwali kwa muda. Kwa sababu ya kiwango kibovu katika hatua za mwisho za kampeni ya 2021-22, Arsenal hawatatarajiwa kucheza kama kikosi chenye kiwango bora ambacho walikuwa wamepata msimu uliopita.

Lakini mwishowe, hadi mwisho wa msimu wa 2022-23, timu zilionekana kuwa sawa na Arsenal. Arsenal hawakuwa katika kiwango bora katika hatua za mwisho za msimu, wakikubali kufungwa na Brighton & Hove Albion na Nottingham Forest. Pia walitoka sare na Liverpool, West Ham United na Southampton.

Kikosi cha Arteta kimepoteza ubora wao kwa sasa na timu za Ligi Kuu sasa zinajua ubora wao. Hii inaweza kufanya mambo kuwa magumu zaidi katika msimu wa 2023-24.

### #1 Shinikizo la matarajio makubwa

Msimu wa Arsenal wa 2022-23 ulikuwa wa kuvutia licha ya ukosefu wa fedha. Kwa sasa wamejiimarisha kama moja ya timu kali zaidi nchini England. Mashabiki watakuwa na matumaini kwamba wanaweza kuiga ushujaa wao katika msimu ujao.


Lakini kuna jambo moja ambalo msimu wa Arsenal wa 2022-23 ilitufundisha, ni kwamba hawafanyi vizuri chini ya shinikizo. Walipoteza uongozi wao wa pointi nane dhidi ya Manchester City mwishoni mwa Machi.

Kwa uzito wa matarajio juu yao, itahitaji azimio na tabia kujihami kwa Arsenal kuwa na msimu mzuri wa 2023-24 kwenye Ligi Kuu England.




## Nukuu

"Nadhani kazi pale Tottenham ni ngumu, na tumeona katika miaka michache iliyopita baadhi ya makocha wakubwa wakihangaika. Ikiwa katika mechi chache za kwanza Spurs hawataanza vema chini ya [Ange] Postecoglou, ninaweza kumuona akiwa katika chini ya presha kidogo," **Nyota wa zamani wa Manchester United, Louis Saha, akitabiri atakayekuwa kocha wa kwanza kutimuliwa Ligi Kuu England msimu huu.**



"Soko bado lipo wazi hadi mwishoni mwa Agosti, nadhani kuna mambo machache au mengi yatakwenda kutokea, tutaona endapo tunahitaji mawinga au wachezaji wa ndani, tutaona nini kitatokea kwa wachezaji wa mkopo, ni wachezaji gani watabaki hapa au la," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akifunguka kuhusu kusajili mbadala wa Riyad Mahrez aliyejiunga na Al-Ahli ya Saudia.**



"Baada ya kumweka katika nafasi hii ya kunyumbulika (mwishoni mwa msimu uliopita), kila mtu alituambia anatakiwa kucheza kabisa katika safu ya kiungo bila kusema kwa nini. Ni nafasi tofauti kabisa na ile aliyocheza msimu uliopita, au aliicheza England, kwa sababu ni nafasi ya kuzuia. Lazima ujipange zaidi. Trent anaweza kucheza nafasi hiyo - inategemea ni nani aliye upande wa kushoto na kulia kwake. Kwa kweli tulifikiri ilikuwa ni jambo zuri na muhimu kulifanya hili katika maandalizi ya msimu mpya," **Jurgen Klopp akifunguka kwamba Trent Alexander-Arnold atatumika kama namba sita Liverpool msimu ujao.**



# KIKOSI BORA CHA USAJILI MPYA KUELEKEA MSIMU WA 2023/24

**Na Adam Fungamwango**

USAJILI wa wachezaji kwa klabu za Tanzania umeendelea kuwa gumzo kwa wiki kadhaa sasa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, ni klabu tatu za Simba, Yanga na Azam ambazo zimekuwa zikitangaza rasmi wachezaji wao pale wanapokuwa tayari wamekamilisha taratibu huku zingine bado zikiendelea kusuasua.

Kabla hata ligi haijaanza, tayari kuna wachezaji wapya wageni waliosajiliwa wameshaanza kutabiriwa kuiteka Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mara nyingi kila msimu kumekuwa na maingizo mapya ya wachezaji wa kigeni ambao pamoja na wengine hawafanyi vizuri, lakini baadhi wanauwasha moto na kuwa vipenzi vya mashabiki wa soka kama ilivyokuwa msimu uliopita kwa Stephane Aziz Ki wa Yanga, James Akaminko wa Azam, Bruno Gomes wa Singida United na Jean Baleke wa Simba ambaye alisajiliwa kwenye dirisha dogo na haikuchukua muda kuingia kwenye vichwa vya mashabiki.

Katika makala haya, Nipashe linakuletea kikosi bora cha wachezaji 11 wapya waliosajiliwa kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu ambao wanatarajiwa kutikisa na kukonga nyoyo za mashabiki.

**#Beno Kakolanya - Singida Fountain Gate**

Pamoja na kwamba bado Singida Fountain Gate hawajamtangaza rasmi, lakini taarifa zinaeleza kipa Beko Kakolanya amesaini na klabu hiyo na ni mmoja wa wachezaji watakaowekwa hadharani kwenye Tamasha la Singida Big Day.

Kakolanya anatarajiwa kuwa mmoja wa makipa watakaotikisa ligi msimu ujao na hapana shaka anakwenda kuwa kipa namba moja kwenye kikosi hicho. Itakuwa hivyo kwa sababu anatoka kwenye klabu kubwa ambayo imecheza mechi mbalimbali za kimataifa na yeye akiwamo, hivyo uzoefu wake utaibeba Singida Fountain Gate katika michuano mbalimbali itakayoshiriki.

**#Kouassi Attohoula Yao - Yanga**

Ameonekana kwenye mechi moja tu siku ya Tamasha la Siku ya Mwananchi ambapo timu ya Yanga ilicheza dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Yao, aliyesajiliwa msimu huu kutoka Asec Mimosas ni raia wa Ivory Coast, pamoja na kwamba aliingia kipindi cha pili, lakini shughuli aliyoifanya ilikuwa ni ishara tosha kuwa patachimbika Ligi Kuu Tanzania Bara itakapoanza.

Ndiye aliyekuja kuchukua nafasi ya Djuma Shaaban anayetajwa kuwa anakwenda kujiunga na TP Mazembe.

**#Cheikh Sidibe - Azam FC**

Ni mchezaji mpya raia wa Mali ambaye mashabiki wa Bongo wataanza kumuona akiwa amevalia jezi ya Azam FC msimu wa 2023/24.

Amesajiliwa kutoka Klabu ya Teungueth ya Senegal na anacheza nafasi ya beki wa kushoto, akiwa anaonekana kuja kuchukua nafasi ya aliyekuwa nahodha wa timu hiyo na kupewa 'thank you' kuelekea msimu ujao, Bruce Kangwa.

Katika mechi ya kwanza ya kirafiki dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan iliyochezwa nchini Tunisia ambapo ipo kwa maandalizi ya msimu ujao, alipachika bao moja, Azam ikishinda 3-0, hivyo anatarajiwa kuuwasha kweli kweli kwenye Ligi Kuu Bara.

**Gift Fred - Yanga**

Kwa waliomuona katika mechi dhidi ya Kaizer Chiefs, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikishinda bao 1-0, aliingia na kufanya mambo makubwa.

Hata hivyo, aina ya uchezaji wake inaonekana ni namba nne, ana nguvu, anapenda kuruka juu kuishambulia mipira mirefu iliyotumwa kwa mawinga na washambuliaji.

Akipata namba tano ambaye ametulia, kazi yake kuiokota mipira ambayo imempita, atakuwa msaada mkubwa kwa Yanga na kutishia namba za watu kwenye kikosi hicho.

**Che Fondoh Malone - Simba**

Ni moja kati ya sajili mpya kwenye Klabu ya Simba ambazo zitaangaliwa na macho mawili na mashabiki wengi wa soka nchini.

Beki huyo wa kati anatarajiwa kucheza pacha na raia wa Jamhuri ya Congo, Inock Inonga.

Anaweza kucheza kama namba nne na tano pia, hivyo watakuwa wanatumana. Malone aliyesajiliwa kutoka Cotonsport ya Cameroon ni raia wa nchi hiyo, ametua kuchukua nafasi ya Mkenya Joash Onyango.

**Fabrice Ngoma - Simba**

Ligi ya Tanzania Bara msimu huu itakuwa na mchezaji mmoja fundi aliitwaye Fabrice Ngoma. Ni mcheaji mwenye uwezo wa kucheza kiungo mkabaji, lakini msaidizi wa kiungo mkabaji maarufu kama namba nane.

Mashabiki wa soka wanataka kuona ufundi wake aliotoka nao AS Vita Club mpaka Al Hilal Omdurman ya Sudan ambako Simba imekwenda kumsajili huko.

**Luis Miquissone - Simba**

Mashabiki wa soka si Tanzania tu, bali Afrika nzima wanataka kuona kama winga huyu atakuwa na ubora ule ule ambao alitoka nao.

Kwa wachezaji wapya waliosajiliwa na Simba msimu huu, matgemeo namba moja ya wanachama na mashabiki ni kwa Luis, raia wa Msumbiji kwa sababu wanaufahamu ubora wake wakati akiichezea timu hiyo msimu wa 2020/21 aliposajiliwa kutoka UD Songo alipokuwa anacheza kwa mkopo kutoka klabu mama ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kabla ya kuuzwa Al Ahly ya Misri 2021. Hapa anachukuliwa kama usajili mpya licha ya kwamba ameshawahi kucheza Ligi Kuu nchini huko nyuma.

**Pacoma Zouzou - Yanga**

Ni kiungo wa kati, namba nane ambaye Yanga ilimsajili kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast. Hakucheza kwenye mechi dhidi ya Kazer Chiefs na sababu bado hazijatajwa, lakini anatarajiwa kuwa mmoja wa wachezaji watakaotikisa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Alassane Diao - Azam**

Moja ya mastraika wapya wa kutazamwa kwenye Ligi ya Tanzania msimu ujao ni Alassane Diao raia wa Senegel.

Amesajiliwa na Azam FC, ikiwa na nia ya kuongezea nguvu safu yao ya ushambuliaji msimu ujao wa ligi.

Ni mmoja wa washambuliaji hatari, mrefu na mwenye nguvu, hivyo anatarajiwa kusumbua mno mabeki wa timu pinzani.

**Hafiz Konkoni - Yanga**

Klabu ya Yanga imemtambulisha straika huyu juzi kutoka Bechem United ya Ghana na yeye pia akiwa ni raia wa nchi hiyo.

Amesajiliwa kuchukua nafasi ya Fiston Mayele ambaye huenda wakati wowote akatambulishwa kama mchezaji wa Pyramids ya Misri.

Hata kama anaweza kuwa siyo kama Mayele, lakini kitendo cha kumaliza nafasi ya pili kwenye ufungaji bora wa Ghana msimu uliomalizika, umbile lake, urefu wake wa futi sita na inchi moja, unaweza kuwa faida kubwa sana kwake kufanya vema kwenye Ligi Kuu kama atautumia vizuri dhidi ya baadhi ya mabeki wa Kibongo wavivu wa kuruka. Tunamuweka kwenye listi hii akicheza pacha na Diao.

**Willy Essomba - Simba**

Wanaomuona kwenye mazoezi nchini Uturuki wanasema ni mchezaji mwenye kipaji wa cha juu na atakuwa midomoni mwa mashabiki mapema tu.

Ni mwepesi, kasi, uwezo wa kupiga chenga na kuingia kwenye eneo la adui kwa haraka sana. Ana uwezo wa kucheza winga zote mbili, lakini hapa anakaa winga ya kushoto. Pia ana uwezo wa kucheza kama namba kumi, msaidizi wa straika namba moja.



Che Malone

**JE, WAJUA?**



KWA mujibu wa mtandao wa ESPN, hawa ndio makocha 10 bora kwa sasa; Pep Guardiola (Man City), Carlo Ancelotti (Madrid), Luciano Spalletti(Hana Klabu), Mikel Arteta (Arsenal), Jurgen Klopp(Liverpool), Lionel Scaloni(Argentina), Erik ten Hag (Man United), Roberto De Zerbi (Brighton), Filippo Inzaghi (Inter) na Xavi (Barca).





# DUWASA kuchukua maji Ziwa Victoria

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendeleza adhma yake ya kutoa maji kutoka Ziwa Victoria, mkoani Mwanza kuyapeleka Dodoma ili kukabili upungufu na kuhakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/2024.

Alisema mpango wa serikali kuyatoa maji katika ziwa hilo hajabadilika kwa kuwa ni moja kati ya mikakati ya kitaifa ya kukabiliana na uhaba wa maji kutokana na ongezeko kubwa la watu na mahitaji ya maji kwa ujumla baada ya serikali kuhamia jijini humo.

"Mipango ya muda mrefu ya kukabiliana na hali hii ya shida ya maji katika mkoa wa Dodoma ni pamoja na kuleta maji ya Ziwa Victoria mkoani Mwanza kuja kutatua kero hii ya ongezeko la mahitaji ya maji ambapo kiasi cha Sh. trilioni 1.2 zinahitajika kwa ajili ya mifumo ya kusafirisha maji," alisema Mhandisi Joseph.

Alisema mpango mwingine wa muda mrefu ni pamoja na ujenzi wa Bwawa la Farkwa, wilayani Chemba, zaidi ya Sh. bilioni 300 zinatarajiwa kutumika kukamilisha mradi huo.

Akizungumza kuhusu hali ya upatikani maji katika Jiji la Dodoma, alisema hivi sasa mahitaji ya maji kwa siku ni lita milioni 133.4 na uwezo wa kuzalisha ni lita milioni 68.7.

"Uzalishaji wa maji hivi sasa katika jiji letu la Dodoma ni asilimia 50 ya mahitaji hivyo upungufu uliopo ni lita milioni 64, hali ambayo inatulazimu kutoa huduma zetu kwa mgao wa saa 13 kila siku na unawafikia asilimia 91 ya watu wote wa Jiji la Dodoma," alisema.

Aidha, alisema ili kukabiliana na hali hiyo, wanaendelea na mikakati mbalimbali kama uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma ikiwamo Kata ya Nzuguni.

Mingine ni kuanzia ujenzi wa miundombinu ya huduma ya majitaka, ikiwamo ujenzi wa mabwawa pamoja na mifumo ambayo itasaidia kumaliza kero iliyopo sasa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, akikabidhiwa mzani na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Vipimo, Dk. Eliza Mwakasangula, baada ya uzinduzi wa bodi ya sita ya wakala huo jijini Dodoma mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waziri aiagiza WMA kuwalinda walaji uhakiki vipimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, ameitaka bodi mpya ya ushauri ya Wakala wa Vipimo (WMA), kuhakikisha walaji wanalindwa kupitia uhakiki wa vipimo, ili wanaponunua bidhaa wapate thamani ya fedha.

Dk. Kijaji aliyasema hayo jijini Dodoma jana alipokuwa anazindua bodi ya sita ya ushauri ya wakala wa vipimo.

Aidha, alimshukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya WMA na wajumbe kwa kuaminiwa na kuteuliwa kwa kuwa wanaunda timu bora inayotoa matumaini makubwa katika kuendelea kusimamia matumizi sahihi ya vipimo kwenye bidhaa pamoja na vifungashio vyake ili wananchi wapate wanachokilipia.

Aidha, waziri aliitaka bodi kufanya kazi yake kwa weledi na kuhakikisha inasimamia usalama wa mali za Watanzania kupitia vipimo sahihi kwa kuwa matarajio ya serikali ni kuhakikisha inatekeleza vipaumbele vya kwenye usimamizi wa matumizi sahihi ya vipimo nchini.

Waziri alisema kupitia usimamizi huo bodi itaweza kuwahudumia wafanyabiashara na wawekezaji na kuishauri serikali kuhusu masuala yote yanayohusu vipimo na kuhakikisha wakala inamlinda mlaji kwa kutumia vipimo sahihi.

Dk. Kijaji aliitaka wakala kuwa pamoja na kazi nzuri wanayoifanya ya usimamizi wa vipimo ni vyema kuendelea kuongeza nguvu katika kusimamia usahihi wa vipimo kwenye maeneo mbalimbali.

Mwenyekiti wa Bodi WMA, Dk. Eliza Mwakasangula, alimshukuru Waziri Kijaji pamoja na Menejimenti ya Wakala na kuahidi kusimamia na kufanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na kushauri wizara ipasavyo kwenye masuala ya vipimo ili kuhakikisha wakala inaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

# NICR yasaini mikataba 48 kuboresha skimu, mabwawa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NICR), imesaini mikataba 48 yenye thamani ya Sh. bilioni 234.1 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa skimu na mabwawa ya umwagiliaji kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23.

Pia imesaini mikataba 22 yenye thamani ya Sh. bilioni 25 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina huku mikataba mitatu kati yake yenye thamani ya Sh. bilioni 23.9 ni kwa ajili ya ununuzi wa magari na mitambo.

Mkurugenzi Mkuu wa NICR, Raymond Mndolwa, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mndolwa alisema wamesaini hati ya makubaliano (MoU) na kampuni mbili kutoka Italia na Hispania kwa ajili ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu.

Kadhalika, alitaja mafanikio ya tume hiyo kuwa ni pamoja na kununua mitambo 15 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji, kununua magari 53 kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya umwagiliaji.

Tume hiyo pia imepata fedha kutoka Benki ya Dunia (WB), kupitia mradi wa PFoR na kwamba utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2023/2024 na gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 70 kwa mwaka. "Tume imefanikiwa kupata fedha kutoka Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), kupitia mradi wa "Irrigation Development Advisory". Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024," alisema.

Akizungumzia mwelekeo wa tume, alisema ni kuendelea kutekeleza miradi itakayoongeza eneo la umwagiliaji lenye ukubwa hekta 256,185.46, ili kufikia hekta 1,200,000 kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2020).

"Mwelekeo wetu mwingine ni huu wa awamu ya tatu ya Mpango Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Awamu ya Pili ya Programu ya kuendeleza sekta ya Kilimo (ASDP II) na kufikia hekta milioni 8.5 ifikapo 2030, ili kufikia malengo tumepanga kutekeleza jumla ya miradi 822, miradi 114 ni ya ujenzi wa mabwawa na 103 ni ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji," alisema.

Alisema maeneo ya kipaumbele katika mwaka wa fedha 2023/2024 ni kukamilisha ujenzi wa skimu mpya 25 zilizoanza kutekelezwa katika mwaka 2022/2023, kukamilisha ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 30 zilizoanza kutekelezwa katika mwaka 2022/2023.

Alisema hatua hiyo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mabwawa 14 yenye mita za ujazo 131,535,000 yaliyoanza kujengwa mwaka 2022/2023, kukamilisha usanifu wa mabonde 22 ya umwagiliaji ulioanza mwaka 2022/2023.


## KUMBUKUMBU



**PATRICK LUCIAN MATERU**
**21/03/1986-31/07/2011**

MPENDWA WETU PATRICK NI MIAKA KUMI SASA TANGU ULIPOTUTOKA GHAFLA ,TULIKUPENDA LAKINI MUNGU ALIKUPENDA ZAIDI. TUNAMSHUKURU MUNGU KWA ZAWADI YA MAISHA YAKO ULIOISHI HAPA DUNIANI UMEKUA MWALIMU MWEMA NA KIONGOZI SHUPAVU, UMETUACHIA ALAMA AMBAYO KAMWE HAITAFUTIKA KATIKA MAISHA YETU ,MAMBO MENGI TUNAYAENZI KUPITIA UPENDO WAKO ULIOTUKA NA TUNAENDELEA KUJIFUNZA MENGI KAMA NJIA YA KUKUENZI.

UNAKUMBUKWA ZAIDI NA BABA,MAMA,KAKA, DADA, NDUGU,MARAFIKI PAMOJA NA WAFANYAKAZI WENZAKO WA WIZARA YA AFYA. TUTAKUKUMBUKA DAIMA MUDA WOTE TULIOKUWA PAMOJA.

*Bwana ametoa na bwana ametwaa jina la bwana lihimidiwe.*
**1 WATHESALONIKE 4:13-18**

## TANGAZO

**BANK OF AFRICA** BMCE GROUP

# TAARIFA YA FEDHA YA BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED YA 30 Juni 2023

Taarifa ya fedha ya Benki iliyochapishwa kwa mujibu wa kifungu na 7 na 8 cha sheria ya Benki na taasisi za fedha ya mwaka 2014

## MUHTASARI WA TAARIFA ZA FEDHA

### MIZANIA

| | Mabadiliko | Jun 23 | Jun 22 |
|---|---|---|---|
| Mikopo Halisi | ↑ 14% | TZS 452.6B | TZS 395.9B |
| Amana za Wateja | ↑ 22% | TZS 549.1B | TZS 448.8B |
| Mikopo Chechefu | ↓ -2.8% | TZS 1.55% | TZS 4.3% |

### MAPATO

| | Mabadiliko | Jun 23 | Jun 22 |
|---|---|---|---|
| Faida (Kabla ya Kodi) | ↑ 88% | TZS 8.9B | TZS 4.8B |
| Mapato Yasiyo ya Riba | ↑ 13% | TZS 12.6B | TZS 11.1B |
| Mapato ya Riba | ↑ 23% | TZS 33.1B | TZS 26.9B |




## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30.06.2023

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Robo ya Mwaka sasa iliyoisha 30 Juni 23 | Robo ya Mwaka Linganishi(Mwaka Uliopita) 30 Juni 22 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Juni 23 | Limbikizo mwaka linganishi 30 Juni 22 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 17,105 | 14,317 | 33,065 | 26,913 |
| 2. Gharama za Riba | (7,361) | (5,573) | (14,646) | (10,391) |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **9,744** | **8,744** | **18,419** | **16,522** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 41 | (862) | 174 | (2,674) |
| **6. Mapato Yasiyo ya Riba:** | **5,370** | **3,987** | **12,594** | **11,141** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,870 | 1,103 | 2,674 | 2,172 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 3,366 | 2,457 | 6,458 | 5,124 |
| 6.3 Gawio | - | 28 | - | 28 |
| 6.4 Mapato Mengine | 134 | 399 | 3,462 | 3,817 |
| **7. Gharama Zisizo za Riba:** | **(11,386)** | **(10,027)** | **(22,252)** | **(20,232)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (5,263) | (4,193) | (9,926) | (8,072) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (895) | (424) | (1,676) | (892) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (5,228) | (5,410) | (10,650) | (11,268) |
| **8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,769** | **1,842** | **8,935** | **4,757** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (1,199) | (552) | (2,904) | (1,427) |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,570** | **1,290** | **6,031** | **3,330** |
| 11. Idadi ya Waajiriwa | 300 | 296 | 300 | 296 |
| 12. Mapato kwa Hisa | 277,680 | 220,559 | 325,815 | 220,559 |
| 13. Idadi ya Matawi | 19 | 19 | 19 | 19 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.3% | 0.8% | 1.6% | 1.0% |
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 11.2% | 6.0% | 13.2% | 7.8% |
| Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 75.3% | 78.8% | 71.8% | 73.1% |
| Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.0% | 6.5% | 5.7% | 6.1% |

## WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2023

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Robo mwaka sasa 30 Juni 23 | Robo mwaka Mwaka linganishi 31 Machi 23 |
|---|---|---|
| **A.MALI** | | |
| 1.Fedha Taslimu | 25,213 | 17,905 |
| 2.Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 39,679 | 52,366 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 147,796 | 134,939 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 7,580 | 10,984 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 7,210 | 8,668 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 38,615 | 96,010 |
| 10. Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 452,645 | 416,636 |
| 12. Mali Nyingine | 14,010 | 17,087 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 1,894 | 1,894 |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Haki ya matumizi ya mali | 7,280 | 7,459 |
| 16. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 8,782 | 8,774 |
| **17. JUMLA YA MALI** | **750,704** | **772,722** |
| **B.DHIMA** | | |
| 18.Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 19.Amana za Wateja | 68,083 | 82,342 |
| 20.Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 471,352 | 478,471 |
| 21.Amana Maalumu | - | - |
| 22. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 77,756 | 80,063 |
| 23. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 24. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 77 | 77 |
| 25. Madeni ya kukodisha | 1,732 | 1,560 |
| 26. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 8,123 | 8,288 |
| 27. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 28. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | - | - |
| Zitakazolipwa Baadae | 3,583 | 4,060 |
| 29. Dhima Nyingine | 16,408 | 16,451 |
| 30. Madeni | 10,868 | 10,868 |
| **31. JUMLA YA DHIMA** | **657,982** | **682,180** |
| **32. MALI/(DHIMA) HALISI (17 kutoa 31)** | **92,722** | **90,542** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 33. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 50,500 | 50,500 |
| 34. Akiba ya Mtaji | 22,242 | 22,242 |
| 35. Mapato Yaliyobakizwa | 11,796 | 11,796 |
| 36. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 6,031 | 3,461 |
| 37. Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 38.Tengo la ongezeko la thamani | 2,153 | 2,543 |
| 39. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **40. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **92,722** | **90,542** |
| 41. Dhima Zisizo Dhahiri | 149,944 | 99,582 |
| 42. Mikopo Chechefu | 7,164 | 7,046 |
| 43. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 10,948 | 10,789 |
| 44. Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.4% | 11.7% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.55% | 1.6% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75.1% | 66.7% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.3% | 53.9% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87.1% | 86.3% |
| (vi) Ongezeko la Amana | -1.7% | -1.2% |
| (vii) Ongezeko la Mali | -2.8% | -0.4% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.06.2023

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Juni 23 | Robo Mwaka iliyopita 31 Machi 23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30 Juni 23 | Limbikizo la Mwaka Linganish (Mwaka Uliopita) 30 Juni 22 |
|---|---|---|---|---|
| **I.Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 3,769 | 5,166 | 8,935 | 4,758 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 2,088 | 1,779 | 3,867 | 6,489 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | - | - | - | (83,303) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (36,936) | 6,490 | (30,446) | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (23,685) | (2,286) | (25,971) | 82,976 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (513) | (104) | (617) | (156) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,194 | (1,933) | 261 | (848) |
| - Kodi Iliyolipwa | (348) | (348) | (696) | (287) |
| -Kiwango cha chini cha tengo la ziada | (131) | (9,740) | (9,871) | (1,427) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(53,562)** | **(976)** | **(54,538)** | **8,202** |
| | | | - | - |
| **II.Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | - |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | 28 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,348) | (1,340) | (2,688) | 3,350 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (12,857) | - | (12,857) | -17,702 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | 1,867 | 1,867 | 16,890 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(14,205)** | **527** | **(13,678)** | **2,566** |
| **III.Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 107 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **107** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (67,767) | (449) | (68,216) | 10,875 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 152,812 | 153,261 | 153,261 | 113,277 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 85,045 | 152,812 | 85,045 | 124,152 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI

(Kiasi kwa millioni shillingi)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ongezeko la thamani | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2023** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **50,500** | **22,242** | **11,796** | **6,425** | **90,963** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 6,031 | - | 6,031 |
| Faida / (Hasara) ya mabadiliko ya thamani | | | - | (4,272) | (4,272) |
| Salio la mwisho wa mwaka 2023 | **50,500** | **22,242** | **17,827** | **2,153** | **92,722** |
| Mwaka Uliopita 2022 | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 2022 | **50,500** | **22,242** | **6,493** | **2,671** | **81,906** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 5,303 | - | 5,303 |
| Faida / (Hasara) ya mabadiliko ya thamani | - | - | - | 3,754 | 3,754 |
| Salio la mwisho wa mwaka 2022 | **50,500** | **22,242** | **11,796** | **6,425** | **90,963** |

| Jina na Cheo: | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Adam Mihayo (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ............................ | 28 Julai 2023 |
| Derick Lugemala (Mkuu wa Fedha) | ............................... | 28 Julai 2023 |
| Alex Kibiki (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ............................... | 28 Julai 2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| Nehemiah Mchechu (Mwenyekiti) | ............................... | 28 Julai 2023 |
| Moremi Marwa (Mkurugenzi) | ............................... | 28 Julai 2023 |

**As strong as a group. As close as a partner.**

# MATANGAZO


## BANK OF AFRICA
BMCE GROUP

## TAARIFA FUPI YA GHARAMA ZA HUDUMA ZETU

| Type of Charge | Product | Charges TZS | FCY (USD, EUR,GBP) |
|---|---|---|---|
| Opening Balance | Corporate Current Account | 250,000 | 500 |
| | SME Current Account | 100,000 | 100 |
| | Personal Current Account | 100,000 | 50 |
| | Faidika Savings Account | 15,000 | 15 |
| | Smart Junior Investor Account | 50,000 | USD 50/ GBP 20/ EUR 15 |
| Minimum Operating Balance | Corporate Current Account | 100,000 | 250 |
| | SME Current Account | 50,000 | 50 |
| | Personal Current Account | 5,000 | 5 |
| | Faidika Savings Account | 10,000 | 10 |
| | Smart Junior Investor Account | 25,000 | Equivalent to TZS |
| | Penalty Below Minimum balance | 12,000 | Equivalent to TZS |
| Minimum Interest Earning Balance | Faidika Savings Account | 1,200,000 | 1,200 |
| | Smart Junior Investor Account | 1,200,000 | 1,200 |
| Ledger Fee | Corporate Current Account | 30,000 | Equivalent to TZS |
| | SME Current Account | 15,300 | 15 |
| | Personal Current Account | 10,300 | 10 |
| | Faidika Savings Account | 1,800 | Equivalent to TZS |
| | Smart Junior Investor Account | nil | nil |
| Withdrawal Charges Over the Counter | **For Corporate & SME** | | |
| | < 15 Million | 2,500 | 1.2% of the amount min 5 |
| | > 15 Million | 1% of the amount max 50,000 | |
| | **For Individuals** | | |
| | < 10 Million | 2,000 | 1% of the amount min 5 |
| | > 10 Million | 0.12% of the amount max 50,000 | |
| Cheques | Cheque Book Issuance-100 leaves | 67,500 | Equivalent to TZS |
| | Cheque Book Issuance-50 leaves | 34,000 | Equivalent to TZS |
| | Cheque Book Issuance-25 leaves | 34,000 | 15 USD/11 EUR/15 GBP |
| | Counter Cheque Leaf for Corporate & SME | 18,000 | 16 |
| | Counter Cheque Leaf for Individuals | 20,000 | Equivalent to TZS |
| | Stop Payment Local Cheque | 1% of total value with min 50,000 and max 250,000 | Equivalent to TZS |
| Statements | Account Statements on Banking Hall per month | 2,000 per page max 100,000 | Equivalent to TZS |
| | E-Statements (Daily, weekly, Monthly, Quarterly) | Free | Free |
| Standing Order | To other Banks | 5,000+ TISS Charges total 15,000 | 15 |
| | Within the Bank | 5,000 | 5 |
| Telegraphic Transfers | TISS (Incoming transfers) | Free | Free |
| | TISS (Outgoing transfers) | 10,000 | Equivalent to TZS |
| | Outward TT- Customer | Equivalent to FCY | $ 54 via Internet Banking, $ 60 without Internet Banking |
| Other Charges | Account Closure | 50,000 | 50 |
| | Dormant Account Activation | Free | Free |
| **TRADE SOLUTIONS** | | | |
| Letters of Credit | **Import LC:** | | |
| | Opening L/C | Equivalent to FCY | 1% pq min 250 |
| | Swift Charges | Equivalent to FCY | 60 |
| | L/C acceptance | Equivalent to FCY | 0.10% |
| | **Export LC:** | | |
| | Confirmation charge - unsecured | Equivalent to FCY | 1.2% min 300 per qtr |
| | Document verification | Equivalent to FCY | 150 |
| | Amendments | Equivalent to FCY | 120 flat fee |
| Bonds and Guarantees | Bid Bond | Unsecured 3.6%; Secured 3%; Cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Performance bonds | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Advance payment | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| | Other guarantees | Secured 3%; Full cash cover 0.6% per qtr | Equivalent to TZS |
| **DIGITAL BANKING** | | | |
| Internet Banking | Subscription | Free | Free |
| | Maintanance Fee | Free | Free |
| | E-Statements | Free | Free |
| | Outward TT | Equivalent to FCY | $54 |
| Mobile Banking | Subscription | Free | n/a |
| | Maintanance Fee | Free | n/a |
| | Balance Enquiry | 200 | n/a |
| | Mini-Statement | 300 | n/a |
| | Full- Statement | 500 | n/a |
| | Fund transfer to other Banks | 10,000 | n/a |
| | Fund transfer to other accounts within BOA | 450 | n/a |
| | Bank to wallet | 1,000 - 49,999 = 2,500<br>50,000 - 99,999 = 3,000<br>100,000 - 199,999 = 3,500<br>200,000 - 499,999 = 5,500<br>500,000 - 1,000,000 = 7,500<br>Above 1,000,000 = 8,500 | n/a |
| | Wallet to Bank | nil | n/a |
| | Forex Rate request | 300 | n/a |
| | Utility Bills Payment | Free | n/a |
| | Airtime Purchase | Free | n/a |
| | SMS Alert | 2500 per Month | n/a |
| Loans | Loan Application Fee | 0.12% of the principal amount minimum TZS 150,000 | Equivalent to TZS |
| | Base/Prime Lending rate | 17% | 8% |

| Cards | | SESAME MAUVE (PURPLE) | SESAME MAUVE (PURPLE) | VISA BLUE | VISA ELITE | VISA GREEN |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Cards | Joining Fees | 0 | 0 | 0 | 0 | 6000 |
| | Card Replacement | 24000 | 24000 | 24000 | 25000 | 6000 |
| | PIN Re-issue | 7500 | 7500 | 6000 | 7500 | 6000 |
| | Block card by Bank | 2500 | 2500 | 2000 | 2000 | 2000 |
| | ATM Cash withdrawal us-on-us | 1300 | 1300 | 1500 | 1500 | 1500 |
| | ATM Cash withdrawal Domestic us-on-them | 1000-99999=1500<br>100000-400000=1700 | 1000-99999=1500<br>100000-400000=1700 | 3000 | 3000 | 3000 |
| | ATM Balance enquiry us-on-us | 400 | 400 | 300 | 300 | 300 |
| | ATM Balance enquiry Domestic us-on-them | 400 | 400 | 600 | 600 | 600 |
| | Cash advance us-on-us | 300 | 300 | 300 | 300 | 300 |
| | Cash advance Domestic us-on-them | 1500 | 1500 | 1500 | 1500 | 1500 |
| | Mini statement us-on-us | 400 | 400 | 600 | 600 | 600 |
| | Mini statement BOA network | 400 | 400 | 1800 | 1800 | 1800 |
| | Failed transactions (Insufficient funds) | 900 | 900 | - | - | - |

BANK OF AFRICA
BMCE GROUP

Benki kidijitali na
**B-Mobile**
*150*13#




**Hamisha pesa**
Hamisha kwenda benki na mitandao yote ya simu

**Nunua LUKU**

**Lipia king'amuzi**

**Salama**
Loki kwa sura au alama za vidole

**Bili ya maji**

**Nunua vocha**

Pakua kutoka App Store Google Play au Piga ***150*13#**


## KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LIMITED (KCJE LTD)

## TANGAZO LA ZABUNI

### ZABUNI NA 1: KCJE/2023-2024/ZABUNI/01: USAMBAZAJI WA MFUMO WA UPIMAJI WA MAZAO PAMOJA NA UNUNUZI WA MIZANI YA KIDIJITALI (2,236), SIMU JANJA (2,236), PRINTA (2,236) NA SOLA (2,236) KWA AJILI YA UPIMAJI WA KOROSHO MSIMU WA 2023/2024

**31/07/2023**

1. "Korosho Cooperative Joint Entreprise Limited" ni Ushirika wa Mradi wa Pamoja ulioanzishwa mnamo tarehe 12 Septemba, 2022 chini ya Kifungu cha 33 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2015. Chama hiki cha Ushirika, kinaundwa na Vyama Vikuu vya Ushirika wa Korosho sita (6) ambavyo ni Vyama Wanachama wake. Vyama hivyo ni pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika MAMCU Ltd (Mtwara), TANECU Ltd (Mtwara), LINDI MWAMBAO Ltd (Lindi), RUNALI Ltd (Lindi), CORECU Ltd (Pwani) na TAMCU Ltd (Ruvuma).
2. Kwa idhini ya "Korosho Cooperative Joint Entreprise Limited" Mwenyekiti wa Bodi, anatangaza Zabuni ya **utekelezaji wa Mfumo wa Upimaji wa Mazao pamoja na ununuzi wa Mizani ya Kidijitali (2,236), Simu Janja (2,236), Printa (2,236), na Sola (2,236) kwa ajili ya upimaji wa korosho za wakulima msimu wa 2023/2024 kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS).**
3. Aidha, Kampuni zenye sifa, vigezo na uwezo wa kutekeleza zabuni hii, zinaombwa kuwasilisha maombi yao kwa kuzingatia sifa mahsusi za mahitaji yaliyoanishwa hapo chini kama ifuatavyo:

**A. SIFA ZA MFUMO WA UPIMAJI WA MAZAO**
- (i) Mfumo wenye uwezo wa kutambua na kuunganisha mzani wa kidijitali na printa;
- (ii) Mfumo uliounganishwa (Integrated) na wenye uwezo wa kutuma taarifa kwenda kwenye "Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU)" pamoja na mifumo mingine ya Serikali;
- (iii) Mfumo wenye uwezo wa kumsajili Mkulima kwa kuchukua picha, alama za vidole pamoja na kuchukuwa ramani ya mashamba;
- (iv) Mfumo wenye uwezo wa kutoa risiti ya karatasi na kielektroniki (SMS);
- (v) Mfumo wenye uwezo wa kutengeneza malipo ya wakulima (Payroll) kwenye Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS) husika;
- (vi) Mfumo uliotengenezwa kwa lugha ya Kiswahili na wenye uwezo wa kufanya kazi hata katika mazingira yasiyo na mtandao na baadae kuweza kutuma taarifa kwa njia ya intaneti na ujumbe mfupi wa maneno (SMS) kwenda kwenye mifumo mingine.

**B. SIFA ZA MIZANI YA KIDIJITALI**
- (i) Mizani ya kidijitali yenye uwezo wa kupima hadi kilo 300 kwa wakati mmoja;
- (ii) Mizani ya kidigitali yenye uwezo wa kuchajiwa kwa njia ya umeme wa jua (Solar DC) na umeme wa kawaida (AC);
- (iii) Mizani ya kidijitali yenye uwezo wa kiusalama usioruhusu kuchakachuliwa (Security features);
- (iv) Mizani ya kidijitali ambayo ina cheti kilichoidhinishwa na Wakala wa Vipimo (WMA Patent Approval).

**C. SIFA ZA PRINTA**
- (i) Printa zenye uwezo wa kuunganishwa na mfumo kupitia RS232, min USB, Bluetooth pamoja na kuunganishwa na mfumo wa Android/IOS; na
- (ii) Printa zenye uwezo wa kutoa taarifa pale karatasi inapoisha, kuchapisha kwa joto (Thermal printer) pamoja na Printa ya Bluetooth.

**D. SIFA ZA SIMU JANJA (SMARTPHONE)**
- (i) Simu janja zenye uwezo wa Android 9.0.
- (ii) RAM: Kuanzia 2GB;
- (iii) Battery: Kuanzia 4000mAh.
- (iv) Kamera kuu: Kuanzia 8MP na 5++ taa kuongeza mwangaza sehemu ambazo kuna mwangaza hafifu.

**E. SIFA ZA SOLA PANEL (UMEME WA JUA)**

| | |
|---|---|
| Power (Pmax): | 5W |
| Power error range: | ±3% |
| Max working current: | 0.27A |
| Max working voltage: | 18V |
| Short circuit current: | 0.32A |
| Open circuit voltage: | 21.67V |
| Working temperature: | -40-65 °C |
| Weight: | 0.55kg |
| Dimension: | 270*180*17mm |

4. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa malipo ya shilingi mia tano elfu tu (500,000/=) malipo hayo yapitie kwenye :-
**NAMBA: 0150771321300**
**JINA LA AKAUNTI: KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LTD BENKI: CRDB – TAWI LA MTWARA**

5. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka mitatau (3) katika kutoa huduma husika.
6. Mchakato wa zabuni hii utafanyika kwa njia shindani ya Kitaifa (NCT) kwa mujibu wa Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya 2016 na ni zabuni ya wazi kwa wazabuni wote wenye sifa stahiki.
7. Wazabuni wote wanakaribishwa ofisi ya Katibu wa Mradi wa Pamoja (Korosho Cooperative Joint Enterprise Ltd) iliyopo Wilaya ya Mtwara Mtaa wa MADUKA MAKUBWA Jengo la Ushirika wa TANECU LTD Ghorofa ya Kwanza kwa ajili ya kuwasilisha maombi muda wa saa za kazi kuanzia saa mbili asubuhi (8:00hrs) hadi saa kumi na nusu jioni (16.30hrs) isipokuwa siku za Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za siku kuu.
8. Wazabuni wote wawasilishe zabuni zao katika Nakala tatu (nakala halisi moja, na nakala kivuli mbili) zikiwa zimefungwa kwa umakini na kuwekwa lakiri. Zabuni zote zitafunguliwa mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha. Tukio ambalo litakuwa la wazi kwa wazabuni na wawakilishi wa wazabuni watakaohudhuria. Mwisho wa kupokea ni siku ya 21/08/2023 saa nne kamili asubuhi (10:00hrs) katika Ukumbi wa Mikutano wa TANECU LTD Mjini Mtwara. Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo: -

**Mwenyekiti wa Bodi,**
**Korosho Cooperative Joint Enterprise Ltd,**
**S.L.P 660,**
**MTWARA**

9. Zabuni zote zitakazochelewa hazitafikiriwa wakati wa tathimini bila kujali sababu zozote za kuchelewa.
10. Zabuni zitakazotuma email, telegram au fax zabuni yake haitafunguliwa wala kufanyiwa kazi.

IMETOLEWA NA

**MWENYEKITI WA BODI**
**KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LTD**
**S.L.P 660,**
**MTWARA**

# LHRC yaanika siri wanawake kuongoza vyombo vya habari

**Na Jenifer Gilla**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, ametaja mambo matatu yatakayowawezesha wanawake kushika nafasi za juu katika vyombo vya habari.

Amesema mambo hayo yanajumuisha kuwapo mikakati imara na endelevu kuwaandaa kushika nafasi hizo.

Lingine ni mafunzo kwa wanawake na wanaume wanaofanya kazi katika eneo hilo, ili kuondoa mifumo dume na imani potofu kuwa mwanamke hawezi kushika nyadhifa hizo.

Mkurugenzi huyo pia ameshauri kubadilishwe mifumo ya kiuongozi na sera, ili iwe rafiki na imsaidie mwanamke kukabiliana na changamoto zitokanazo na jinsia wakati anatekeleza majukumu yake.

Dk. Anna aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam alipofungua mafunzo ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari wanawake yaliyoandaliwa na Umoja wa Wachapishaji wa Magazeti Duniani (WAN-IFRA) kupitia programu ya Women in News (WIN).

Programu hiyo ni maalum kwa ajili ya waandishi wa habari wanawake katika nchi mbalimbali duniani, ambao hukuzwa kuelewa masuala ya uongozi, usawa wa kujinsia, kukabili rushwa ya ngono, pia hutoa mafunzo kwa vyombo vya habari vyenye ushirikiano navyo katika nchi mbalimbali.

Alisema kundi hilo linashindwa kupenya katika nafasi za juu za uongozi kutokana na mifumo dume inayowadhoofisha na kuwaondolea ari ya kujiamini licha ya kuwa na uwezo wa kushika nafasi hizo.

"Na jambo hili linaanzia nyumbani - malezi wanayopewa watoto wa kike yanawaandaa kuwa wake na watoa huduma wa familia na sio kuwa wanataaluma, hali hiyo inawanyima fursa ya kuonesha uwezo wao katika masuala ya maendeleo," alisema.

Dk. Anna jambo lingine linalowarudisha nyuma wanawake ni ukatili wa kijinsia na kukiri kuwa ni moja ya makundi yanayokwenda katika kituo chao kutafuta msaada wa kisheria ili kujiokoa na tatizo hilo.

"Ukatili wa kijinsia ni mkubwa katika vyombo vya habari na unachangia wanawake kutoshika nyadhifa za juu kwa sababu wanaotakiwa kuwaandikia barua za kuonyesha uwezo wao, wanataka wapewe rushwa ya ngono kwanza," alisema.

Mkurugenzi wa WAN-IFRA, Kanda ya Afrika, Jane Godia, alisema wameandaa mafunzo hayo kwa lengo la kuwajenga uwezo waandishi hao, ili kuwaongeza kujiamini na kuomba nafasi za juu zinapotangazwa.

Alisema lengo la shirika hilo ni kuondoa tofauti kubwa ya uongozi iliyoko katika ya wanawake na wanaume katika vyombo ya habari kwa kuwa utafiti unaonesha kuwa ni asilimia 10 tu ya wanawake nchini wameshika nafasi hizo.

Aliwashauri waandishi wa habari wanawake kutumia fursa ya kukua kwa teknolojia kukuza na kutangaza taaluma zao.

Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alisema ili kuongeza nafasi za uongozi kwa wanawake katika taaluma hiyo, wanapaswa kuandaliwa taratibu, kutiwa moyo na kupatiwa msaada kisaikolojia pale wanapopitia changamoto za kiuongozi.

Aliwashauri waandishi wa habari wanawake kutokatishwa tamaa na changamoto za kiuongozi wanazokumbana nazo badala yake wazitumie kama fursa ya kuwa bora zaidi ikiwamo kujiendeleza kielimu.

Akiwakaribisha wageni hao kwa niaba ya Mwenyekiti wa WIN Alumn, Salome Kitomari, mwanachama Vumilia Mwacha alisema kuna jumla ya wanachama 78 waliopatiwa mafunzo mbalimbali huku wengine wakiendelea na mafunzo ya uongozi.

Alisema wana WIN kokote waliko katika vyombo vya habari wameendelea kufanya vizuri kitaaluma na kiuongozi na kwamba mafunzo ya mara kwa mara yameendelea kuwajenga katika kuondoa mfumo dume na kuongeza sauti za wanawake kama vyanzo vya habari, viongozi wa vyombo vya habari na wanaoendelea kufanya kazi ya uandishi wa habari.




Wafuasi wa madhehebu ya Shia, wilayani Muheza, mkoani Tanga wakiwa katika matembezi ya amani ya kumbukumbu ya kifo cha Imamu Hussen- mjukuu wa Mtume Mohamad (SAW) aliyeuawa Iraq mwezi 10 Muharram mwaka 61 Hijiria wakati akitetea dini ya Kiislam. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wafanya matembezi kuomboleza kifo mjukuu wa Mtume Muhammad

**Na Selemani Mpochi**

JUMUIYA ya Khoja Shia Ithanasheri nchini imefanya matembezi ya kumbukizi ya Siku ya Ashuraa ambayo Imam Hussain (a) - mjukuu wa Mtume Muhammad (s) aliuawa huko Karbalaa, Iraq mwaka 61 A.H (miaka1300 iliyopita).

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Muhammedraza Dewji, alisema wanakumbuka siku hiyo kwa kuwa inafundisha kuishi kwa mujibu wa maadili mema katika jamii kokote ulimwenguni.

"Dhamira yetu kubwa ni kueneza maadili hayo mema yaifikie jamii ya wanadamu wote bila kujali dini zao au taifa la mtu. Wanaofanya matembezi wanaamini kuwa mjukuu huyo wa Mtume Muhammad (s) alisimama kwa ajili ya ubinadamu na kwa wanadamu wote na si vinginevyo," alisema Muhammedraza.

Mwenyekiti huyo alisema wanaamini hivyo kwa sababu utamaduni wa wanadamu kwa asili umesheheni misingi ya utu na maadili mema.

Alisema kuvunjika au kupuuzwa kwa misingi hiyo katika zama hizo, ndiko kulikomfanya imam Hussain (a) akubali kutoa maisha yake ili kuinusuru misingi hiyo ya ubinadamu duniani.

Baada ya matembezi hayo, Muhammedraza alisema matembezi hayo ni kwa ajili ya watu wote, bila kujali itikadi za kidini wala siasa.

Jumuiya ya Khoja Shia Ithanashari ni ya Kiislamu ambayo mbali na kutoa huduma za kiroho, pia inatoa misaada mbalimbali ya kibinadamu kwa Watanzania bila kujali dini au kabila.

Ndani ya mwezi huu wa Muharram, jumuiya hiyo ilitarajia kuchangia damu kwa ajili ya wagonjwa wanaohitaji kuchangiwa damu salama.

# Viongozi mikoa, wilaya waagizwa kutatua migogoro ya wananchi

**Na Ibrahim Joseph, RUVUMA**

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul, amewataka viongozi wa ngazi ya mikoa na wilaya kushughulikia kero na migogoro mbalimbali ya wananchi iliyoko katika maeneo yao ili kupunguza mzigo kwa serikali.

Gekul aliagiza hayo mwishoni mwa wiki baada ya kupokea malalamiko ya wananchi wa Kijiji cha Liuli, Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma akiwa katika mikutano yake ya kampeni ya kutoa elimu ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia. Wananchi walilalamikia uongozi wa kijiji kupora ardhi.

Aliwataka viongozi hao kuanzia ngazi ya mtaa hadi mkoa kuhakikisha wanafika kwa wananchi kusikiliza na kutatua kero katika maeneo yao ili serikali isilaumiwe.

"Kampeni hii imefanikiwa kufika hadi ngazi ya mtaa kusikiliza malalamiko na kero za wananchi. Zipo kero za kisheria, wataalamu wameshauri lakini zipo zingine za kiutendaji, hivyo viongozi washughulike na ukitajwa kiongozi kuhusika ujifakari kama unatosha kwenye nafasi uliyonayo," alisema.

Kuhusu Mwenyekiti wa Kijiji kutuhumiwa kupora mashamba ya wananchi, Gekul alisema atalikabidhi kwa ngazi husika za chama na serikali ili hatua zichukuliwe.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Mzee Victory Luena alimtuhumu mwenyekiti wa Kijiji chao kupora mashamba yake yenye ukubwa wa ekari 12 ambazo alidai amekuwa akizimiliki tangu mwaka ya 1974.

Luena alidai mwenyekiti huyo kwa kushirikiana na Ofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) walimzuia kuendeleza eneo hilo kwa madai limebadilishwa matumizi.

"Mheshimiwa hapa kijijini kwetu mwenyekiti wetu amegeuka kuwa mwizi wa maeneo. Ameanza kutupora ardhi yetu kwa nguvu na kunitishia kuwa ataniua na kuchoma moto nyumba yangu lakini mimi siogopi hilo. Ninachodai hapa ni mali yangu, ni mwizi huyo hapo kama anabisha aseme," alidai.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Liuli, Ezekiel Haule, alisema hahusiki na kupora mashamba ya wananchi hao.

Haule alisema eneo ambalo amelichukua, lilikuwa halijaendelezwa, hivyo wanachosema wananchi wenzake dhidi yake ni uongo.

# Jaji Mkuu asema wanajipanga utekelezaji hoja Tume ya Samia

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema tayari mahakama zimeanza kujipanga kufanyia kazi mashauri yatakayotokana na upelelezi bora kutoka Taasisi za Haki Jinai kwa kuzingatia mapendekezo ya tume iliyoundwa na Rais katika upelelezi na ukusanyaji wa ushahidi wa kisayansi.

Prof. Juma aliyasema hayo mjini Morogoro mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Mwaka wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania.

Alisema kutokana na maendeleo makubwa ya teknolojia, Tume ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai imeainisha maeneo ambayo wananchi wameagiza taasisi zote katika mfumo wa Haki Jinai yaboreshwe na kubadilishwa, jambo ambalo Mahakama ya Tanzania itaguswa na kuhusika na maboresho yatakayofanyika katika taasisi zingine za haki jinai.

Alitolea mfano wa eneo lililoguswa linalohusu hatima ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambapo tume ilibaini kuwa taasisi za haki jinai zinakabiliwa na changamoto ya mifumo kutosomana.

Jaji Mkuu alisema Mahakama ya Tanzania haiwezi kuyakwepa mapendekezo ya tume hiyo ya kuwapo mfumo jumuishi wa haki jinai unaosomana utakaounganisha Taasisi za Haki Jinai utakaosaidia katika kubadilishana taarifa.

"Kutokana na mfumo mpya wa mahakama wa usimamizi, ni lazima tujitayarishe kuungana, kusomana na kubadilishana taarifa na mfumo tarajiwa wa Taasisi za Haki Jinai nchini," alisema Prof. Juma.

Alisema mahakama haitoeleweka kwa jamii ikishindwa kupokea na kutumia ushahidi wa kisayansi utakaodhalilishwa na mifumo bora ya kiupelelezi itakayojengwa.

Alisema Mahakama ya Tanzania ni miongoni mwa taasisi zilizoangaliwa na tume hiyo ambayo imetoa mapendekezo yake kuhusiana na masuala iliyobaini na yanayohitaji maboresho, ikiwamo mashauri kuchukua muda mrefu mahakamani bila kusikilizwa.

"Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman, wananchi wanalalamikia sana kuhusu mashauri yaliyokwama kwa muda mrefu katika mahakama zetu bila kusikilizwa," alisema Prof. Juma.

Jaji Mkuu alitumia nafasi hiyo kuwataka watumishi wa mahakama kusoma ripoti hiyo ili kujiwekea utamaduni wa kufuatilia kwa ukaribu mabadiliko yanayotokea nje ya mahakama, ikiwamo matumizi ya teknolojia za kisasa.

Pia aliwapongeza majaji na watumishi wengine wa mahakama hiyo kwa kutimiza wajibu wao Kikatiba kuhusu utoaji haki kwa mafanikio makubwa.

Alisema taarifa ya Msajili Mkuu ya Mwaka 2022, inaonesha Mahakama ya Rufani ilimaliza jumla ya mashauri 1,890 ambayo ni mengi zaidi ya yale yaliyomalizika mwaka 2021. Yalikuwa 1,879.

Msajili Mahakama ya Rufani, Silvester Kainda, alitaja baadhi ya mambo yatakayojadiliwa ni pamoja na kupata taarifa na takwimu za mashauri kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia Januari - Desemba 2022, wingi wa mashauri na uwezo wa mahakama kumaliza mashauri.

Kainda alitaja eneo lingine la kubadilishana uzoefu kuhusu uendeshaji wa mashauri ya Mahakama ya Rufani, kupata taarifa ya mkakati wa maboresho ya Mahakama ya Tanzania na hali ya mifumo ya TEHAMA kuelekea Mahakama Mtandao (ECMS).

Lingine ni taarifa ya tathmini ya bajeti ya mwaka 2022/23 na maandalizi ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 na kupata uelewa wa masuala mbalimbali kuhusu afya ya akili na msongo wa mawazo na namna bora ya kukabiliana nayo.



Mkurugenzi wa Mambo ya Ndani wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Ndositwe Haonga, akipewa maelezo na ofisa wa mamlaka hiyo kuhusu matumizi ya mfumo wa kuhakiki stempu ya kielektroniki (ETS) unavyofanya kazi katika kuskani stempu za vinywaji kama maji, juice, pombe kali na sigara, alipotembelea banda la TRA katika maonesho ya Sabasaba yaliofanyika mwezi uliopita Dar es salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Majaliwa awapongeza Watanzania kushiriki Kongamano la Uchumi Urusi

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewapongeza wafanyabiashara 19 kutoka Tanzania walioshiriki maonesho ya kibiashara katika Jukwaa la Kimataifa la Uchumi na Kibinadamu la Afrika na Urusi yaliyofikia tamati Julai 28, mwaka huu.

Wafanyabiashara hao wanamiliki kampuni zinazohusika na sekta za elimu, afya, kilimo, madini, mafuta na gesi, utalii, ujenzi, utafiti na ushauri wa kibiashara.

Alitoa pongezi hizo juzi alipozungumza nao jijini St. Petersburg, Urusi ambako alimwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Pili wa Kilele baina ya Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka mataifa ya Afrika na Urusi.

"Ninawapongeza kwa kuamua kusafiri na kuja hadi huku ili kutumia fursa ya mkutano wa Urusi na Afrika kutafuta masoko ya bidhaa zenu na wabia wa kufanya nao biashara kule nyumbani. Sekta binafsi ya pande zote mbili za nchi yetu ni muhimu. Ninataka mtambue kuwa mna mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu," alisema.

"Udhahiri wa sekta binafsi umeonekana leo kwa kitendo chenu cha kushiriki Expo Forum na mimi ninataka niwathibitishie kuwa mnao uwezo mkubwa wa kutafuta mitaji na rasilimali mbalimbali.

"Niwasihi muungane mkono ili mweze kuwafikia wazalishaji wakubwa huku mkiwaeleza kuwa Tanzania ni nchi iliyokaa kimkakati katika sekta ya kibiashara," alisema.

Aliwaambia wafanyabiashara hao kwamba serikali inathamini majukumu yao na kwamba itawaunga mkono ili waendelee kufanya vizuri.

Pia aliwapa nafasi wafanyabiashara hao watoe maoni yao kuhusu ushiriki wao katika Jukwaa la Kimataifa la Uchumi na Kibinadamu ili serikali ifanyie kazi.

Mapema akisoma risala kwa niaba ya wenzake, Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Otieno Igogo, alisema walikuja na bidhaa mbalimbali ili kuzitangaza na kutafuta fursa za kibiashara katika soko la Urusi.

Alizitaja bidhaa hizo kuwa ni korosho, mafuta ya alizeti, kahawa, rosella, viungo mbalimbali (spices), mchele, karanga, vanilla, madini mbalimbali, zabibu na mvinyo.

Igogo alimweleza Waziri Mkuu kwamba kampuni 10 kati ya 19 zilizoshirki kongamano hilo kutoka Tanzania, zimetia saini mikataba ya ushirikiano wa kibiashara na kampuni 11 za Urusi. Kampuni zingine tano ziko katika maongezi ya ushirika wa kibiashara.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mashariki, Balozi Mbarouk Mbarouk, Naibu wa Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Ally Suleiman Ameir, Balozi wa Tanzania Urusi, Fredrick Kibuta na watendaji wengine wa serikali.

## Wakulima wafurahia nyongeza bei mahindi

**Na Francis Godwin, IRINGA**

WAKULIMA wa mahindi mkoani Iringa wameanza kunufaika na bei mpya ya Sh. 950 kwa kilo iliyotolewa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), baada ya serikali kuweka ruzuku ili kuwapunguzia mzigo wakulima.

Tofauti na miezi mitatu iliyopita kilo moja ilinunuliwa kwa Sh. 650 hali iliyowafanya wakulima kupaza sauti na serikali kuagiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na CPB kununua mazao hayo ili kuwaepusha wakulima na ulanguzi.

Meneja wa CPB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Jaspa Samweli alimweleza mwandishi wa habari hizi jana ofisini kwake kuwa ongezeko la wakulima wakubwa na wadogo kuuza mahindi kwa sasa ni kubwa zaidi, kwa kuwa limesaidia kuongezeka kwa ununuzi wa mahindi.

Aidha, alisema vituo vya ununuzi ni Songea mkoani Ruvuma, Mlowo na Tunduma Mkoa wa Songwe pamoja na Iringa .

Alisema, CPB imeanza kununua mahindi mwezi mmoja uliopita kwenye kituo cha Iringa kwa kilo moja Sh. 950 wakati Kituo cha Songea ni Sh. 850, Mlowo na Tunduma mkoani Songwe kilo moja ni Sh. 850.

Aidha, alisema hadi sasa zaidi ya tani za mahindi ya wakulima 13,500 zimenunuliwa ikiwa ni kati ya tani 80,000 zinazotarajiwa kununuliwa kutoka kwa wakulima ndani ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Dk. Samweli alisema kutokana na ongezeko kubwa la wakulima kukimbilia kuuza mahindi yao CPB Iringa wamelazimika kuweka utaratibu wa kununua gunia moja hadi tani mbili na wale wakulima wakubwa wa tani saba kuendelea lengo ni kuhakikisha makundi yote yanafikiwa.

Alisema kwa wote wanaofika kuuza mahindi yao kuwa viwango vya ubora wa mahindi yanayotakiwa kununuliwa hivyo kabla ya ununuzi mahindi yanapimwa maabara na yale yaliyokidhi viwango yananunuliwa kisha mkulima anawekewa fedha kwenye akaunti ya benki ndani ya siku tatu.

Kwa mujibu wa Dk. Samweli, tangu watangaze utaratibu huo kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wakulima kwa kuwa wanaona kuna ongezeko zuri ikilinganishwa na Sh. 650 waliyonunua kwa wanunuzi binafsi.

Alisema CPB ina jumla ya vipimo 12 vya kupima ubora wa mahindi yanayonunuliwa kuendena na soko la mahindi la Afrika Mashariki ili kuepuka kulichafua Taifa kwa kupeleka mahindi ama unga usio na ubora katika soko la Afrika Mashariki.

"Uandaaji wetu wa mahindi toka kwenye ununuzi hadi usagaji ni wenye viwango vya soko la Afrika Mashariki ambao unatumiwa na nchi zote za Afrika Mashariki. Mfano unga unaotoka CPB ni wenye virutubisho vyote na usio na madhara ya sumu kuvu," alisema.

Alisema kama mahindi ama unga ama maharage na mazao mengine yanayotoka Tanzania yakipelekwa nje ya nchi na kubainika kuwa na tatizo aibu hiyo siyo ya wakulima ama CPB pekee yao bali ni kwa taifa na ni wajibu wa kila Mtanzania kutunza taswira ya nchi yake.

HABARI MICHEZO

# KIDUKU AKIRI MSAUZI KUMZIDI, MANDOGA ATUPIA USHIRIKINA

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI Bondia wa Ngumi za Kulipwa nchini, Twaha Kiduku, akikiri kuzidiwa mambo mengi ya kiufundi na mpinzani wake, Asamahle Wallem kutoka Afrika Kusini na kwamba ndiyo sababu ya kuchezea kichapo juzi, Karim Mandonga yeye ametaja ndumba ndizo zimesababisha kupigwa.

Mabondia hao waliopigana walipanda ulingoni jijini Mwanza juzi ambapo Kiduku alikuwa akiwania ubingwa wa WBF dhidi ya Wallem huku Mandonga akichezea kichapo kwa KO dhidi ya Mganda Moses Golola.

Kiduku alipoteza pambano hilo la raundi 12 la uzani wa Super Middle kwa pointi ambapo alikiri hakuwa na siku nzuri kazini dhidi ya mpinzani wake huyo kutoka Afrika Kusini aliyekuwa moto kweli.

Bondia Kiduku alianguka chini katika raundi ya tatu, lakini aliweza kuinuka na kuendelea na pambano hilo baada ya kuhesabiwa ingawa hakuweza kumudu makonde ya mpinzani wake, kutokana na kutawaliwa katika raundi zote kabla ya majaji kumpa ushindi Msauzi huyo, hivyo kushindwa kutetea mkanda wake wa WBF.

Akizungumza baada ya pambano hilo, Kiduku alisema amepoteza pambano hilo kwa kuwa haikuwa siku yake nzuri kazini huku akikiri kuzidiwa mbinu nyingi na mpinzani wake.

"Sikuwa na siku nzuri leo na wala haikuwa bahati, nimepoteza mbele ya mpinzani mzuri ambaye amenizidi mambo mengi, naenda kujipanga naamini nitarudi nikiwa bora zaidi, " alisema Kiduku.

Kwa upande wa Mandonga, alisema ameshindwa dhidi ya Golola, kutokana kuletewa bondia wa ajabu akiwa na waganga wa jadi.

Hilo ni pambano la pili kupoteza kwa Mandonga baada wikiendi iliyopita kupokea kichapo kwa pointi mbele ya Daniel Wanyonyi nchini Kenya.

Alisema haelewi wapinzani ambao amekuwa akiletewa, wengine wamekuwa kama waganga wa kienyeji kutokana na mambo wanayomfanyia kabla ya pambano lenyewe.

"Ni kweli nimepoteza pambano, binafsi sielewi nimepoteza vipi kwa sababu upande wa mpinzani wangu tangu siku ya kupima uzito nilikuwa simwelewi kabisa, amekuja na mashuka na mikoba kama mganga wa jadi ila niwaambie kwa sasa atakayekuja awe kibwengo au mganga wa jadi, ajue nitapita naye tu bila ya wasiwasi," alisema Mandonga.

Mapambano mengine yaliyopigwa siku hiyo ni Juma Misumali ambaye alifanikiwa kumchapa Paul Kamata wakati Joseph Mchapeni akimshinda kwa TKO raundi ya kwanza Agustine Michael, Ayubu Mwakina amemchapa George Odongo, Mohamed Mkude akimchapa Seba Temba huku Juma Chamamba akishinda kwa TKO ya raundi pili mbele ya James Ebelo.

KIKAPU...




Mchezaji wa timu ya mpira wa kikapu wa Dynamos, Seleman Khamis, akijaribu kufunga goli huku akizongwa na wachezaji wenzake wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ihefu yatumia Samia Cup kujiandaa Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Ihefu FC kimeamua kushiriki michuano ya Mbeya Samia 'pre season' Cup inayofanyika wilayani Kyela kwa ajili ya kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Themi Felix, amesema wameamua kushiriki michuano hiyo kwa ajili ya kuwaweka wachezaji wao fiti kabla ya kuanza kwa Ligi Kuu msimu wa 2023/24.

Michuano hiyo imeandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homela, na inazishirikisha timu mbalimbali za Mbeya, ikizialika pia timu kutoka Zambia, ikiwamo Nakonde Town Council.

"Kikubwa tunaendelea na maandalizi yetu na sasa tupo kwenye michuano hii, hizi mechi ni sehemu ya maandalizi yetu kabla ya kwenda kwenye ligi kwa hiyo tumeyapa heshima kubwa kuleta kikosi cha kwanza, kikiwa na wachezaji wa zamani na wapya tuliowasajili kwa ajili ya msimu ujao wa ligi," alisema Themi.

Naye kipa mpya wa timu hiyo, Hussein Masalanga, alisema michuano hiyo imeanza kuwaweka fiti kimwili na kiakili na ana uhakika mpaka ligi itakapoanza watakuwa wapo sawa.

"Mashindano ni mashindano tu, ni tofauti na mechi za kirafiki, yanatusaidia wachezaji kupambana ili kusaka ushindi wakati huo huo tukijiweka fiti kimwili na kiakili kwa ajili ya mapambano yajayo, tunajua msimu ujao ni mgumu. Tumepata mashindano kama haya, hivyo naamini yatatusaidia ili kikosi chetu kiwe vizuri," alisema.

Wakati timu mbalimbali zikiwa zimesafiri maeneo mbalimbali kwa ajili ya 'pre season', Ihefu imeamua kuweka kambi Kyela ikishiriki michuano hiyo na kuifanya kuwa ndiyo mechi zake za kujipima nguvu kabla ya kuanza mikikimiki ya ligi hapo Agosti 15, mwaka huu.

## Mtoto wa Choki atua bendi ya Mapacha Music

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya muziki wa dansi ya Mapacha Music, imeongeza safu ya uimbaji kwa kuwachukua waimbaji chipukizi Choki Junior na Punda Junior.

Wanamuziki hao chipukizi ni watoto waimbaji wakongwe wa muziki wa dansi nchini, Ally Choki na Mhina Panduka.

Akizungumzia na gazeti hili, mmiliki wa bendi hiyo Jose Mara, amesema amewachukua ili kukuza vipaji vyao, na kwamba tayari wameshaanza kuonyesha uwezo wa kuimba.

"Unajua mtoto wa nyoka ni nyoka tu, hivyo vijana wameshaanza kuonesha vipaji vyao vya kuimba muziki na wamekuwa na mchango katika bendi," alisema Mara.

Amesema vijana hao watashiriki kurekodi nyimbo mpya zinazoandaliwa na bendi hiyo kwa ajili ya albamu mpya kwa mwaka huu.

Amezitaja nyimbo ambazo wanajiandaa kuzirekodi kuwa ni 'Chozi la Mwanaume na Hukumu ya Penzi', ambapo amefafanua kuwa kufikia Septemba zitakuwa zinasikika hewani.

## Rais ZFF ataka soka la kulipwa

**Na Saada Akida**

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Suleiman Jabir, amesema anapambana kurejesha heshima ya soka visiwani humo kutoka la ridhaa na kulifanya kuwa la kulipwa.

Amesema kazi kubwa ni kutoa semina na mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa klabu na timu zote za visiwani Zanzibar, Uguja na Pemba.

Akizungumza na Nipashe jana, Jabir alisema baadhi ya klabu na timu nyingi za Zanzibar hazina ofisi maalum, sababu inayochangia kukosa wadhamini wa kuziwezesha klabu hizo kujimudu kwa kufanya usajili mzuri na kuleta makocha kutoka nje.

Alisema timu ambazo zimefanikiwa kujiendesha kisasa ni zile zinazomilikiwa na taasisi kama ilivyo kwa KMKM, Mafunzo na JKU, ambazo zimekuwa zinafanya usajili na kuketa wachezaji kutoka mataifa mengine.

"Tunahitaji kurejesha soka la Zanzibar kuwa la ushindani, kwa klabu kupata wadhamini kama ilivyo kwa Bara, hatuwezi kufika huko hadi kuwapo kwa mafunzo ya utawala bora kwa viongozi, kwa kuziondoa timu kwenye majumba yao na kuwa na ofisi maalum," alisema Jabir.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL ipo kwenye mazungumzo na Paris St-Germain kuhusu kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kukataa uhamisho wa rekodi ya dunia wa pauni milioni 259 kwenda Klabu ya Saudi Arabia Al-Hilal. **(Sunday Mirror)**

### REAL MADRID NA MBAPPE

KLABU ya Real Madrid imeweka kikomo cha kima cha euro milioni 230 kumnunua Kylian Mbappe kutoka Paris St-Germain kwa mkataba wa kudumu. **(Marca)**

### LAVIA AWANIWA LIVER

LIVERPOOL inabakia kwenye mazungumzo na Southampton kuhusu kiungo wao wa kati wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 19, baada ya kuona dau la awali la pauni milioni 34 pamoja na pauni milioni nne za nyongeza zimekataliwa**. (Liverpool Echo)**

### JAY Z KUINUNUA SPURS

MWANAMUZIKI nguli, Jay-Z anajiandaa kuinunua Tottenham Hotspur ikiwa mmiliki wa klabu hiyo, Joe Lewis atapatikana na hatia kwa madai ya ulaghai na utoaji wa taarifa za ndani za kampuni kunakochukuliwa kuwa kinyume cha sheria. **(Express)**

### TRAORE ATAKIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inapanga kumnunua winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 27, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Wolves. **(Football Insider)**

### BAYERN YAMGANDA KANE

BAYERN Munich inabakia na uhakika wa kukamilisha dili la kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30, kabla ya dirisha la usajili kufungwa. **(Sky Sports)**

### TEN HAG KUFIKIRIA UPYA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amelazimika kufikiria upya mipango ya kumuuza mchezaji wa kimataifa wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 26. **(Telegraph)**

### MANE NA LIVERPOOL

LIVERPOOL inatazamiwa kukosa pauni milioni 7.5 za nyongeza zinazolipwa kutoka Bayern Munich iwapo mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 31, ataondoka katika klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na kujiunga na Klabu ya Saudia ya Al-Nassr. **(Mail)**

### LAPORTE KUONDOKA CITY

MLINZI wa Hispania, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 29, ataondoka Manchester City ikiwa watakamilisha usajili wa beki wa kati wa Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21, kutoka RB Leipzig. **(Manchester Evening News)**

### MARQUINHOS LULU PSG

KLABU ya Paris St-Germain imekataa matarajio ya kumuuza mlinzi wa Brazil, Marquinhos mwenye umri wa miaka 29, huku klabu zikiwamo Al-Nassr zikivutiwa nae. **(RMC - in French)**

### DE BEEK KUPIGWA BEI

KLABU ya Real Sociedad imeanza mazungumzo na Manchester United ili kumnunua kiungo wao wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, 26. **(AS)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: LIGI YA SAUDIA IMEBADILISHA SOKO LA USAJILI

**Hakuna aliyefikiria kuwa wachezaji wengi wa juu zaidi wangeenda kucheza...**

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ameionya Ligi Kuu England kwamba fedha zinazotolewa nchini Saudi Arabia 'zimebadilisha soko' baada ya kumpoteza winga, Riyad Mahrez kwenda Al Ahli.

Mahrez ni mmoja wa nyota wakubwa ambao wamemfuata Cristiano Ronaldo Mashariki ya Kati msimu huu wa majira ya joto.

Akiwa hakutarajia kumpoteza Mahrez msimu huu wa majira ya joto, Guardiola amesisitiza kuwa City haitatafuta mbadala wa moja kwa moja wa Mualgeria huyo, lakini akakiri kwamba fowadi wa aina yake hawezi kufika Etihad.

"Hatutafuti mbadala wa Riyad katika suala la ustadi kwa sababu kila mchezaji ni tofauti," alisema Guardiola.

"Tutaona kitakachotokea kwa wachezaji wa mkopo na ni wachezaji gani watakaa hapa. Mambo machache yatafanyika."


Guardiola aliendelea kuwaonya wachezaji wengine wa Ligi Kuu England kwamba matumizi ya fedha kwenye Ligi Kuu ya Saudia yamebadilisha sana soko la uhamisho na kuziacha hata timu kubwa za England zikishindwa kushikilia vipaji vyao vya juu.

"Saudi Arabia imebadilisha soko," alieleza. "Miezi michache iliyopita, wakati Cristiano ndiye pekee aliyeondoka, hakuna aliyefikiria kuwa wachezaji wengi wa juu zaidi wangecheza kwenye Ligi ya Saudia.

"Katika siku zijazo kutakuwa na zaidi na ndiyo maana klabu zinahitaji kufahamu kinachoendelea. Riyad alipata ofa ya ajabu na ndiyo maana hatukuweza kusema 'usifanye'."

City, wakiwa wamempoteza pia nahodha Ilkay Gundogan aliyejiunga na Barcelona msimu huu wa majira ya joto, wanamenyana na Bayern Munich ili kumbakisha beki wa kulia Kyle Walker, ambaye amepokea ofa kutoka kwa mabingwa hao wa Bundesliga.

# BARCELONA YAIKAMUA MADRID MAREKANI




**TEXAS, Marekani**

OUSMANE Dembele, chipukizi Fermin Lopez na Ferran Torres waliifungia Barcelona wakati ikiichapa Real Madrid mabao 3-0 kwenye El Clásico katika Uwanja wa AT&T mjini Arlington, Texas nchini Marekani Jumamosi.

Dembele mwenye umri wa miaka 26, ambaye ESPN imeripoti kuwa anakaribia kuhamia Paris Saint-Germain, aliiweka Barca mbele katika dakika ya 15, akitumia pasi ya Pedri na kumtungua kipa Thibaut Courtois.

Madrid waligonga mwamba mara tano, tatu kupitia kwa Vinicius Junior, walipokuwa wanatafuta bao la kusawazisha kabla ya mchezaji wa akiba Lopez mwenye umri wa miaka 20, kufunga bao la kushangaza na Torres akaongeza la tatu.

Miamba hao wawili wa Hispania wanamaliza ziara zao za Marekani wiki hii, Barcelona wakicheza na AC Milan huko Las Vegas Jumanne, na Madrid watamenyana na Juventus huko Orlando, Florida Jumatano.

Kocha wa Barca, Xavi Hernandez na mwenzake wa Madrid, Carlo Ancelotti, walichagua timu zenye nguvu, huku wachezaji waliosajiliwa majira ya joto, Ilkay Gundogan na Oriol Romeu wakianza kwa Barca, na Jude Bellingham akiwamo kwenye kikosi cha kwanza cha Madrid.

"Ulikuwa mchezo mzuri ambao tulicheza, tukiwa na mpira tuliwakandamiza, tulipata nafasi, mwendo mwingi," alisema Ancelotti.

"Kitu kibaya ni matokeo, mwisho tulikuwa tunashambulia sana, tukiwa hatuna uwiano wa kutosha, matokeo yanaumiza, lakini nitazingatia mazuri tuliyofanya, kwa ujumla timu ilicheza vizuri, tulipata nafasi nyingi."

# Hojlund ni suala la muda tu Man Utd

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imekubaliana ada na Atalanta kwa ajili ya uhamisho wa mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund, kwa mujibu wa 90min.

Msako wa mshambuliaji kwa 'Mashetani Wekundu' hao msimu huu wa majira ya joto uliwaongoza kwa fowadi huyo wa zamani wa Sturm Graz, ambaye alifunga mabao tisa katika mechi 32 za Serie A msimu uliopita.


Ofa ya hivi majuzi zaidi ya United ilikataliwa na Atalanta kabla ya Paris Saint-Germain kuingia kwenye zabuni na pendekezo la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

90min sasa inaelewa kuwa ofa ya mwisho kutoka kwa Man United ina thamani ya euro milioni 85 ni katika nyongeza zinazowezekana.

Maslahi binafsi yalifikiwa kati ya pande hizo mbili mapema Julai na mkataba wa miaka mitano na United wanatarajia kuhitimisha dili hilo haraka ili aweze kushiriki katika maandalizi yao ya msimu mpya.

Hojlund hakuhusika katika mechi ya kirafiki ya Atalanta na Bournemouth Jumamosi, lakini kusainiwa kwa mbadala wake - El Bilal Toure wa Almeria - kumetangazwa na timu ya Italia.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark, Hojlund atakuwa wa tatu kuwasili United majira haya ya joto baada ya kiungo Mason Mount na kipa Andre Onana.




# Boca Juniors yamsajili Cavani


**BUENO AIRES, Argentina**

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani, amejiunga na Boca Juniors baada ya kusitishwa kwa mkataba wake na klabu ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Valencia, klabu hiyo ya Argentina imetangaza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, ametia saini mkataba wa miezi 18, huku Boca ikiomba muda wa ziada kutoka kwa FA ya Argentina ili kumsajili mshambuliaji huyo kwa hatua ya 16 ya Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini).

"Tumefurahi kuwa na Cavani nyumbani," klabu hiyo yenye maskani yake Buenos Aires iliandika kwenye mtandao wa kijamii wa X, ambao zamani ulijulikana kama Twitter, pamoja na video ikimkaribisha mchezaji huyo.

Cavani, ambaye alianza maisha yake ya soka akiwa na Danubio ya Uruguay, alihamia Ulaya mwaka 2007 alipojiunga na Palermo.



Baada ya misimu minne alihamia Napoli, ambako alifunga mabao 104 katika michezo 138 na kushinda Coppa Italia.

Mwaka 2013, alisajiliwa na Paris Saint-Germain, ambapo alicheza kwa miaka saba, na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa klabu - rekodi ambayo alishikilia hadi msimu uliopita wakati fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe alimpita kwa kufunga mabao 212 katika mashindano yote.

Alishinda mataji sita ya Ligue 1, mataji matano ya Ufaransa na mataji sita za ligi jijini Paris pamoja na medali ya washindi wa pili katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Cavani alijiunga na Manchester United mwaka 2020 kabla ya kuhamia Valencia kwa uhamisho wa bure miaka miwili baadaye. Klabu hiyo ya Hispamia ilikubali mapema Jumamosi kusitisha mkataba wa mshambuliaji huyo, ambao ulikuwa unamalizika mwakani.

Cavani amecheza mechi 136 na kuifungia Uruguay mabao 58 na kuwa mfungaji bora wa pili nyuma ya Luis Suarez. Aliisaidia nchi yake kushinda taji la Copa America mwaka 2011.

## Simba kumtema kipa Mbrazili

INATOKA UKURASA 24

kwenda sawa kabla ya dirisha la usajili kufungwa, unajua kilichosababisha hadi wamkate ni majeruhi ya mara kwa mara na vipimo vimeonesha, ndiyo maana viongozi wanapambana kupata mbadala wake kwa haraka.

"Ni jambo ambalo uongozi umeamua kulifanya siri kwa sababu tayari Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Salim Abdallah 'Try Again', alifika juzi nchini Uturuki na kukabidhi majina manne ili kuchagua jina moja la kipa ambaye atakuja kuchukuwa nafasi ya kipa huyo Mbrazili.

"Zoezi hili linatakiwa kukamilika ndani ya siku moja na kesho (leo) kuwahi dirisha la usajili wa CAF ambalo linatarajiwa kufungwa saa 6:00 usiku," kilisema chanzo hicho makini.

Kwa upande wa Robertinho, alipoulizwa hakutaka kuweka wazi juu ya suala hilo zaidi ya kuongelea kambi ya timu yake ilivyokuwa nchini Uturuki.

"Tumefanyia kazi mambo mengi katika kipindi hiki, ikiwamo utimamu wa miili, umoja, ushirikiano, mbinu na mifumo tutakayoitumia mara kwa mara katika mechi zetu za ndani na kimataifa, kwa wachezaji kuonekana kuelewa kwa haraka zaidi, hayo mengine siwezi kusema chochote," alisema Robertinho.

## Yanga na sababu kumsajili Konkoni

INATOKA UKURASA 24

"Kwanza mchezaji anaweza kusema pamoja ya kwamba nina mkataba wa mwaka mmoja, lakini sitaki kubakia hapa, hivyo klabu inatafuta thamani ya mchezaji halafu ofa zinakuja zinasikilizwa anauzwa, au klabu yenyewe inafanya tathmini na inaamua kumuuza japo ana mkataba, au mnakaa na kukubaliana kuvunja mkataba sasa haya mambo siyo ya kuyafanya kihuni tu," alisema Kamwe akifafanua kwa nini suala hili limechukua muda mrefu kukamilika huku mchezaji huyo na Djuma Shaaban wakitaka kuondoka muda mrefu.

Akimzungumzia Mayele alisema kuwa naye jambo halijakamilika kama lilivyokuwa la Bangala na likishakamilika wataliweka wazi.



# DSTV YAJA NA SOKA PROMAX, EPL, LA LIGA, SERIE A NDANI

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa soka nchini wametakiwa sasa kukaa mkao wa kula baada ya SuperSport kutangaza rasmi kuwa kupitia DStv itaonyesha mubashara michuano maarufu ya kandanda ulimwenguni zikiwamo Ligi Kuu kubwa na maarufu kama EPL, La Liga, Serie A pamoja na mashindano ya UEFA.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, katika uzinduzi wa msimu mpya wa soka unaofahamika kama 'Premier League ni Soka Pro Max!', Kaimu Mkuu wa Masoko wa DStv Tanzania, Semu Bandora, alisema msimu huu ni moto wa kuotea mbali na Watanzania hawataachwa nyuma kwani wataweza kushuhudia michuano hiyo mubashara ndani ya DStv.

"Kwa hakika huu ni msimu wa soka ProMax! Na tunamaanisha hivyo kwani sisi DStv tutaonesha michuano hiyo laivu na kutufanya na sisi Watanzania tuwe sehemu ya soka la ulimwengu," alisema Semu na kuongeza kuwa kitimtim hicho kitaanza Agosti 6 kwenye Ngao ya Jamii na mtifuano utaendelea Agosti 11, mwaka huu vumbi la Ligi Kuu ya England (EPL), litakapoanza rasmi kutimka.

Alisema ili kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wanashuhudia na kufurahia michuano hiyo, timu maalum ya watangazaji na wachambuzi wa michezo kwa lugha ya Kiswahili watatangaza na kuchambua michuano hiyo akitaja miongoni mwao ni Jemedari Said, Geoff Lea, Ahmed Abdallah, Edgar Kibwana, Ibrahim Masoud 'Maestro', Abubakar Liongo na George Ambangile.

Bandora alisema kama hiyo haitoshi, DStv Tanzania pia imetoa ofa kabambe kwa wale ambao bado hawana visimbuzi vyao ambapo kwa sasa watapata kwa ofa maalum ya Sh. 59,000 vikihusisha dikoda ya DStv pekee pamoja na kifurushi cha Shangwe kwa mwezi mmoja.

Aidha, aliwataka Watanzania kuchangamkia ofa hiyo ili wasipitwe na burudani ya soka ya ProMax kwani DStv lengo lakini ni kutaka kuona kila mteja akifurahia burudani hiyo ya soka.

Alisema kwa mteja wa kifurushi cha DStv Poa, Bomba na Shangwe, ataweza kushuhudia mechi mbili kwa wiki za Ligi Kuu ya England huku mteja wa DStv Compact yeye akishuhudia mechi zote 380 za ligi hiyo.




Baadhi ya wachambuzi wa michezo kwa lugha ya Kiswahili watakaotangaza na kuchambua michuano ya msimu mpya wa Ligi ya England, Jemedari Saidi (kushoto), Ibrahim Masoud 'Maestro' (katikati) na Geoff Leah, wakizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa Kampeni ya 'Premier League ni Soka ProMax' ndani ya DStv, iliyofanyika katika viwanja vya TPDC Jumamosi iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Pindi mgeni rasmi Singida Big Day J'tano*

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha Tamasha la Singida Big Day linalitarajiwa kufanyika Jumatano ijayo katika Uwanja wa Liti, ambapo pia utapigwa mchezo wa kirafiki kati ya timu Singida Fountaine Gate na AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Makamu wa Rais wa Klabu ya Singida Fountain Gate, Ibrahim Milambo, amesema kila kitu kimekwenda kama kilivyopangwa na wanatarajia kufanya tamasha hilo



ambalo anaamini litafana kutokana na ukubwa wa maandalizi.

"Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Pindi Chana, tunatarajia kuwapokea AS Vita Club hapa Singida, najua wameshawasili hapa nchini, vile vile uwanja upo kwenye hali nzuri hasa sehemu ya kuchezea kwa hiyo mashabiki watapata burudani safi siku hiyo ambayo itakuwa rasmi kwa ajili ya kuwatambulisha wachezaji wetu wa zamani na wapya tuliowasajili tutakaowatumia kwa msimu ujao wa mashindano," alisema Makamu rais huyo.

Ofisa Habari, Hussein Massanza, alisema wameshavunja kambi yao iliyokuwa jijini Arusha na wamerejea Singida tayari kwa tamasha hilo.

"Tumeshavunja kambi, tumeondoka Arusha, tumerudi nyumbani na sasa tunajiandaa na tamasha letu la Agosti 2, niwaambie mashabiki wa Singida Fountaine Gate kuwa mbali na pambano la soka kati yetu dhidi ya AS Vita Club, kutakuwa na burudani mbalimbali, atakuwapo Dulla Makabila ambaye ni mkali ya singeli, hivyo mashabiki wote wa muziki huo watakuwa na furaha sana siku hiyo, lakini pia msanii Nandy na timu yake watatupatia burudani kwenye tamasha letu," alisema.

Singida Fountaine Gate ambayo ilicheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu uliopita, imefanikiwa kukata tiketi ya kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

# Michezo

Jumatatu Julai 31, 2023
Nipashe



Boca yamsajili Cavani UKURASA 22

## Yanga na sababu kumsajili Konkoni

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema Hafiz Konkoni ndiye straika waliyekuwa wanamhitaji baada ya kufanya upembuzi yakinifu kutokana na bechi la ufundi kuridhishwa naye na si mwingine.

Klabu hiyo pia imesema haitomsajili mchezaji yeyote kwa kelele au presha za mashabiki.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Ali Kamwe, amekiri pia kuwa wamemuuza kiungo Yannick Bangala kwenye Klabu ya Azam FC, huku akisema ukimya waliokuwa nao ulitokana na kumfanyia tathmini mchezaji ambaye walikuwa na mkataba naye.

"Tumemsajili straika huyu kutoka Benchem United FC na ndiye tuliyekuwa tunamfuatilia na si yule Mcameroon ambaye mlikuwa mnamtoa sana kwenye vyombo vya habari na kumfanyia promo, tulikuwa tunafuatilia wenyewe taratibu, hizi promo za hawa wachezaji wengine ambao mlikuwa mnazipiga kuwahusisha na klabu yetu miaka ya nyuma ilikuwa inasababisha klabu zetu kuingia mkenge na kusajili tu kwa sababu ya presha za mashabiki," alisema Kamwe.

Awali, kulikuwa na taarifa kuwa klabu hiyo ingemsajili straika Emmanuel Mahope ambapo ilielezwa kuwa dili lilivunjika dakika za mwisho kwa sababu ya kutaka mshahara mkubwa, lakini kwa mujibu wa Kamwe ni kwamba hawajawahi kuwa kwenye mipango ya kumsajili straika huyo.

Akizungumza kuhusu uhamisho wa Bangala, Kamwe alisema kama klabu wamefanya biashara kwa sababu bado alikuwa na mkataba wa mwaka mmoja.

"Kwa faida ya mashabiki wote wa soka, wachezaji wenye mikataba ni tofauti sana na wale ambao wamemaliza mikataba kama kina Benard Morrison au Eric Johora wale walikuwa wamemaliza mikataba na ndiyo maana imekuwa rahisi kuwaambia 'thank you', lakini hawa wengine waliokuwa na mikataba zipo hatua za kupitia kwanza.

INAENDELEA UKURASA 23



# Simba kumtema kipa Mbrazili

**Na Saada Akida**

## Vipimo vya afya vyabainisha tatizo, Robertinho asugua kichwa aletewa Msovenia na wengine...

HATIMAYE Klabu ya Simba imefikia uamuzi wa kuvunja mkataba na kipa mpya wa ndani ya timu hiyo, Mbrazili Jefferson Luis, kwa kile kilichoelezwa ni kushindwa kufaulu vipimo vya afya alivyofanyiwa nchini Uturuki licha ya kuwa tayari ameshajiunga na timu hiyo hali iliowafanya kuanza kusaka mbadala wake katika mataifa ya Ulaya, imefahamika.

**Julai 23, mwaka huu Simba ilitangaza kumsajili kipa huyo kutoka Resende ya kwao Brazil kwa lengo la kuziba pengo la kipa namba moja wa timu hiyo, Aishi Manula, ambaye anauguza majeruhi yake bega baada ya kufanyiwa upasuaji.**

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya uongozi wa klabu hiyo, zimeeleza suala la kipa huyo limekuwa likifanywa kwa usiri kuwa hatokuwa mmoja kati ya wachezaji wa timu hiyo inayotarajia kuingia nchini kesho kutoka Uturuki baada ya kuvunja mkataba wake kutokana na vipimo vya afya alivyofanyiwa nchini humo.

Aidha, taarifa hizo zimeenda mbali zaidi baada ya kueleza kuwa viongozi wa timu hiyo tayari wameshawasiliana Kocha Mkuu wa timu hiyo, Robertinho Oliveira kwa kumpa majina ya makipa kutoka katika mataifa manne likiwamo Taifa la Slovenia inayopatikana barani Ulaya kwa ajili ya kupitisha jina moja ili kumalizana naye kabla kufungwa kwa dirisha la usajili.

"Jefferson hana uhakika wa kuja nchini kwa sababu amefeli vipimo vya afya na uongozi kwa sasa unapambana kumpata mbadala wake ili kuweza

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >